# Nipashe

Alhamisi Novemba 23, 2023 • Tanzania 1000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581503

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com



www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





MDAU UASISI MKATABA PARIS – AENDELEZA VIKAONI COP...

**Mapya ya Samia kunakishi mzizi wa JK na tabianchi nyumbani hadi kimataifa**

•Pia yumo penye sauti 'mama na mazingira'




UKURASA 11

**DAWASA** yaja na mfumo wa kulipia maji kabla kutumia

UKURASA 4

**WAZANZIBAR** waitwa kujiandikisha katika daftari la wapigakura

UKURASA 17



**MASHAMBULIZI** yaongezwa Gaza, Afrika Kusini kuitenga Israel

UKURASA 19

VITA YA UWEKEZAJI

# JK ang'aka USA, China

**ATOA** angalizo kwa viongozi wa Tanzania diplomasia ya uchumi...

*Endelea Ukurasa wa 2*




Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete

## MASHINE MAALUM VVU YAZINDULIWA

UKURASA 3



Abiria zaidi ya 200 wanaosafiri kutoka mjini Muheza, mkoani Tanga kwenda vijiji vya Kicheba, Misozwe na maeneo mengine, wakiwa wamekwama kuendelea na safari baada ya maji ya Mto Mkurumuzi kupita juu ya daraja **(picha ndogo)** na kukata mawasiliano kutokana na mvua iliyonyesha jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

UKURASA WA 2

## MIKOPO ASILIMIA 10 YAREJESHWA, PM AONYA VIKALI

MIKOPO ya halmashauri kwa makundi maalum sasa inarejea baada ya kusitishwa na serikali. Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kuwa ifikapo Januari 15 mwakani, halmashauri zote zirudi katika utaratibu wa kuitoa.

Waziri Mkuu aliagiza hayo...

## Wakuu nchi za Afrika Mashariki wateta Arusha

UKURASA 8

**MICHEZO** YANGA KURUDIA YA USM ALGER KUIMALIZA CR BELOUIZDAD KWAO UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Kikwete ang'aka 'vita' uwekezaji USA, China

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



RAIS mstaafu Jakaya Kikwete ameeleza uzoefu wake katika diplomasia ya uchumi, namna alivyohimili kutoegemea upande wowote kwenye uwekezaji na biashara kimataifa nchini.

Mstaafu huyo akafafanua kuwapo msuguano kati ya uwekezaji wa Kichina na Kimarekani, lakini daima akadumu kwenye ufanisi wa biashara na uwekezaji unaoivusha Tanzania.

Huku akiwataka viongozi wa sasa kufuata nyayo hizo, Kikwete, maarufu JK, ameongezea mbinu nyingine aliyotumia, utafiti na ushauri wa kitaalamu ulikuwa mtaji wake mkubwa kufanikisha uchumi.

Kikwete ambaye kitaaluma ni mchumi, aliyasema hayo jana jijini hapa alipofungua Kongamano la Kitaaluma la Maendeleo ya Biashara na Uchumi lililoandaliwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

"Watu wanapiga kelele kweli, 'China...' Siku moja nilikuwa na Wamarekani, wananiambia tatizo ni China," akatamka na kufafanua ulivyokuwa mrejesho wake kwao, kwamba:

"Hamuwataki Wachina tu? Nchi zetu zinatafuta uwekezaji, Wachina wanaleta uwekezaji, Wamarekani wapo, Waingereza wapo, Warumi wapo, Waajemi wapo. Nchi zetu zinatafuta masoko ya bidhaa zetu China, Uingereza, Marekani tunapata."

Kuhusu utafiti, Kikwete aliweka angalizo kwamba hakuna mbadala kwenye suala hilo na kinyume chake nchi haitakuwa ya uhakika wa kuvuka kuelekea katika maendeleo.

Alikumbusha alivyotumia kada ya wasomi kumvusha, alipowatengea asilimia moja ya bajeti ya nchi kuwekeza katika utafiti wa miradi, akitoa mfano wa mapinduzi kwenye Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), akinyooshea kidole Kituo cha TARI Naliendele kilivyompatia mrejesho chanya.

Alisema kwenye michakato ya uwekezaji, suala la kukutana na misuguano hiyo ya mataifa makubwa kiuchumi ni kawaida, muhimu ni kwa viongozi wa Kitanzania kusimamia maslahi ya nchi pasipokuwa sehemu ya mivutano hiyo.

Kikwete alitetea hoja yake kwa mfano wa ziara yake ya hivi karibuni kwenye Kiwanda cha Toyota China. Alikuta bendera za Marekani, Japan, China na mataifa mengine yaliyowekeza huko.

"Kiwanda kinazalisha magari 200,000 kwa mwaka na walisema magari haya tunauza hapahapa China, hakuna hata moja linalotoka.

"Meneja aliyejitambulisha kwangu ni raia wa Japan, akasema 'tuna viwanda vitatu vya namna hii'. Sasa wao wamewekeza, lakini Mchina akija kuwekeza huku shida, yaani kama vile wanataka wao wakawekeze lakini sisi tusinufaike," alisema.

Katika simulizi hiyo, Kikwete alisema uzoefu unaonesha kwenye uzalishaji simu aina ya Iphone inayotoka China, akisisitiza usipokuwa mwelevu na kutambua yanayoendelea, watakubana wakati wao ndio wawekezaji wakubwa China na wamesaidia kujenga uchumi wa taifa hilo.

"Umoja wa Mataifa, ile Taiwan ilikuwa inawakilisha China. Baba wa Taifa alikuwa mstari wa mbele kuipigania haki ya China, baadaye kampeni ile ilifanikiwa na ndio msingi wa urafiki wa China na Tanzania.

"Kwanini nchi za Afrika kufanya biashara na China iwe tatizo? Lakini sisi tunahitaji msaada wa maendeleo. Wamarekani wanatoa na China wanatoa, sasa kuna tofauti gani?

"Lakini wakubwa hawawataki, mnaulizwa hawa Wachina vipi? Kitu cha muhimu ni kuwaambia 'ninyi mna matatizo na China, sisi hatuna matatizo wala ugomvi nao. Mnataka sisi turithi ugomvi wenu?' Mnachogombania nini? Sisi hatujui, mnajua wenyewe huko katika ukubwa wenu, lakini nchi za Afrika zenyewe kuna vitu inavyovitafuta hiki na hiki, yeyote atakayetupa fursa hiyo, sisi tutafanya naye shughuli'," alisema.

Alisisitiza maendeleo yanachochewa na matumizi sahihi ya utafiti na ushauri wa kitaalamu na katika jamii yenye matumizi madogo ya utafiti, nchi hiyo huwa nyuma kimaendeleo. Na ndio sababu Afrika iko nyuma kimaendeleo.

"Pale Samsung, pale kazi yao ni utafiti. Kama hamwekezi kwenye utafiti, huwezi kukua. Nilipokuwa Rais, nilitembelea vituo vyote vya utafiti. Kwanza nikakuta watu wote wazee nikauliza 'kwanini?' Wakasema ni kwa sababu ajira zilisimamishwa.

"Nikawaambia sasa la kufanya nikasema 'hamtastaafu, mtaendelea kufanya kazi hadi pale utakapochanganya viini vya maharage na mahindi, tutasema wewe sasa kalee wajukuu'," alisema Kikwete na kuibua vicheko kwa washiriki wa kongamano hilo.

Kuhusu mazingira ya uwekezaji nchini, Kikwete alisema ili nchi ikue, inahitajika kutengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji na biashara ili watu wavutike kuwekeza.

"Tunapozungumzia watu kuvutika kuwekeza si wa nje tu, bali pia wa ndani na nje. Kukiwa na mazingira magumu ya biashara, hata wa ndani hawawekezi, wanakimbia.

"Si siri, siku moja nilikwenda Afrika Kusini, nikamkuta marehemu Zacharia Hanspope, biashara yake nikamkuta akasema na magari yangu nimehamishia huku, nikamwuliza sababu ni nini, akasema pale nyumbani mazingira ya uwekezaji hayajakaa sawa," alisema.

Alisisitiza kuwa ili uchumi ukue, lazima kuwapo uwekezaji na hakuna uchumi utakaokua, lakini wawekezaji hawapendwi.

"Hakuna uchumi unaoweza kukua bila uwekezaji, uwekezaji unastawi kwenye mazingira ya biashara ambayo ni mazuri, uwekezaji ni bidhaa ambayo inaona aibu kuwapo mahali ambapo si rafiki.

"Ukitengeneza mazingira ya biashara yasiyokuwa rafiki, wapya wanaogopa kuja na waliopo wanaondoka na kama hawaondoki hawajitanui kibiashara wanasema 'ngoja tuangalie inavyokwenda maana huna hakika kesho yako itakuwaje," alisema.

Alieleza kuwa anaamini katika kongamano hilo yatazungumzwa mazingira ya uwekezaji yalivyo ili kutoa ushauri kwa serikali juu ya kile kizuri cha kuyafanya na kuendeleza na kile kisicho kizuri kirekebishwe au kiachwe.

"Tukifanya hivyo ndugu zangu ndivyo uchumi utakavyokua, hata ukizungumza unataka ajira, ajira zinazalishwa na uchumi unaokua, uchumi usiokua hakuna ulichoongeza na ajira hakuna," alionya.

Kikwete aliongeza, "mtangoja waliozeeka wastaafu na sasa hivi wazee wenyewe ni kama sisi, hivi kila ukitiona unadhani bado vijana, huwa wanarudi kwenye mafaili kule wanasema walikosea kuandika mwaka wa kuzaliwa.

"Nilipokuwa waziri, nilikuwa ninayapata sana hayo, unaambiwa baba yake alikosea kuandika mwaka, vijana wanakaa wanasubiri ajira hazipatikani," alisema Kikwete na kusababisha vicheko zaidi.

Alisema wajibu wa serikali ni kutengeneza mazingira ya sekta binafsi kukua na kugusia kuwa wakati wa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) waliangalia mazingira ya biashara na kila walipokutana katika Baraza la Mawaziri walijadili.

"Mjadili na mwangalie kwa kina mchango wa biashara, uvumbuzi katika mageuzi ya kiuchumi ya nchi yetu, nimevutiwa na mada zilizopo kama uboreshaji na urahisishaji mazingira ya biashara katika kutoa ajira kwa vijana," alisema.

Hata hivyo, alisema endapo mada za kongamano hilo zitajadiliwa ipasavyo na wadau na serikali ikafanyia tafakuri ya kina na mapendekezo yake, kongamano hilo litakuwa chachu ya kuchagiza maendeleo makubwa ya kiuchumi nchini.

Alitoa rai CBE kuandaa makongamano hayo kwa kushirikiana na taasisi nyingine kwa kuwa mawazo, ushauri na mapendekezo yatakayotolewa na kufikisha kwa wadau na serikali yatakuwa na uzito mkubwa.

## Mikopo ya asilimia 10 yarejeshwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MIKOPO ya halmashauri kwa makundi maalum sasa inarejea baada ya kusitishwa na serikali. Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kuwa ifikapo Januari 15 mwakani, halmashauri zote zirudi katika utaratibu wa kuitoa.

Waziri Mkuu aliagiza hayo jana jijini Arusha wakati akizindua wiki ya Maadhimisho ya Huduma za Kifedha Kitaifa na kusema kuwa utaratibu wa zamani ulisitishwa katika utoaji mikopo kwa vikundi kwa kuwa baadhi ya taratibu zilikiukwa na serikali iliagiza kuwapo utaratibu mzuri wa utoaji mikopo kupitia huduma za kifedha.

Alisema toka ilipotangazwa kusitishwa na serikali, ana uhakika umewekwa utaratibu mzuri wa vikundi kunufaika na fedha hizo, hivyo ifikapo Januari 15 mwakani, ukopeshaji kwa vikundi uwe umeanza.

Waziri Mkuu alisema serikali ilikuwa inatoa fedha nyingi katika vikundi hivyo, lakini kuna baadhi ya watumishi ambao sio wema, walikuwa wanatumia mwanya wa utaratibu mbovu kujinufaisha. Sasa mianya hiyo imefungwa na vikundi vya jamii hiyo vitakuwa vikinufaika ifikapo mwakani.

Akizungumzia wiki ya maadhimisho hayo, Majaliwa aliitaka Wizara ya Fedha kuhakikisha elimu inatolewa hasa maeneo ya vijijini kwa njia za sinema, matangazo kwa njia ya mitandaoni, vyombo vya habari vya kidigitali, redio na televisheni.

Majaliwa alisema asilimia 53.8 ya watumiaji huduma ya fedha iliyopo sasa haitoshi kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa elimu ya huduma hiyo haijawafikia wananchi wa vijijini, hivyo kuna wajibu wa wizara ya fedha kujikita huko, ili kuinua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Waziri Mkuu aliikumbusha wizara hiyo kuhakikisha inazingatia na kutekeleza mipango ya maendeleo kwa Taifa kwa ajili ya kuinua uchumi wa nchi.

Vilevile, alizitaka taasisi zote za fedha zitambulishe mahali zilipo, ili wajasiriamali wadogo na wa kati wakopesheke kwa lengo la kukuza mitaji yao na kujikwamua kiuchumi.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema amefurahishwa na maandalizi ya maadhimisho hayo kwa kuwa yanatoa fursa kwa wadau wa taasisi za kifedha kutoa elimu kwa wananchi kutumia huduma za kifedha.

"Kutokana na maadhimisho haya Watanzania watanufaika na elimu hii kwa kuwa watapata elimu ambayo itawasaidia kuongeza kipato na kukua kiuchumi," alisema.

Waziri huyo alisema jamii ikiwa na uelewa sahihi wa elimu ya huduma za kifedha itawasaidia wananchi kutokukopa mikopo umiza na kuingia mikataba ambayo itawabana pasipo kutambua kwa kuwa wengi wao hawasomi mikataba hiyo, bali hukimbilia kutia saini na kuchukua fedha bila kusoma na kuielewa.

"Watanzania wengi hatuna nidhamu ya mikopo na tunakopa kwa malengo yaliyokusudiwa, lakini tukichukua fedha tunaishia kuzipeleka katika matumizi yasiyokuwa rasmi na baadaye kujutia wakati wa urejeshaji mikopo hiyo,"alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Natu El-maamry, alisema maadhimisho hayo ya tatu ni mwendelezo wa jitihada za serikali katika kuongeza uelewa wa masuala fedha kwa Watanzania ili waweze kuwa na uelewa kuhusu matumizi sahihi ya huduma za kifedha.

Alisema taasisi mbalimbali za kifedha na wadau wa kisekta wanatumia kipindi hiki kutoa elimu na huduma kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

Natu alisema maadhimisho hayo yameandaliwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na wadau wa huduma za kifedha. Benki 35 na kampuni za simu nchini zimeshiriki.



Wananchi wakiangalia lori la mizigo lililobeba bidhaa ya unga wa ngano, lililopinduka katika eneo la Vigwaza-Chamakweza, mkoani Pwani jana. Kwa mujibu wa mashuhuda wa ajali hiyo, lori hilo lilipoteza mwelekeo baada ya kugusana ubavuni na basi la abiria la Kamwana wakati wakipishana, ambapo watu wawili wamejeruhiwa na wengine watatu wanadaiwa kupoteza maisha. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Mbaroni tuhuma udhalilishaji watoto Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar linawashikilia watu 14 kwa tuhuma za vitendo vya udhalilishaji, ikiwamo kuwaruhusu watoto wa kiume kuingiliana wenyewe kwa wenyewe, ulawiti na ubakaji.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake visiwani hapa. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Richard Mchumvu, alisema watuhumiwa hao wamekamatwa katika maeneo mbalimbali ya mkoa na utaratibu wa kuwafikisha mahakamani unaendelea.

Kukamatwa kwa watuhumiwa hao kunatokana na taarifa za watoto watatu wa kiume katika maeneo tofauti kutoa taarifa ya kulawitiwa na watu mbalimbali katika vituo vya polisi.

Alivitaja vituo walivyoripoti matukio hayo kuwa ni Ng'ambu, Fuoni, Mazizini, Bubu na Madema, vyote viko katika mkoa wa Mjini Magharibi.

Kamanda Mchomvu alisema waliendesha msako maalum katika maeneo ya Raha Leo, Kisauni, Fuoni, Bububu, Malindi, Magomeni Jitini ambayo yanadaiwa kuhusika na vitendo hivyo na umri wa vijana waliolawitiwa ni wa miaka 15 hadi 17.

"Watuhumiwa wawili kati ya 13 tunaendelea na uchunguzi dhidi ya ushiriki wao katika makosa hayo," alisema Kamanda Mchomvu.

Alitaja majalada yaliofunguliwa kuhusiana na matukio hayo ya udhalilishaji ni tisa kati ya hayo, manne upelelezi umekamilika na yamepelekwa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua zaidi. Alisema majalada matano yanaendelea na upelelezi na kuahidi kuwa ukishakamilika, watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

Katika uchunguzi wa awali, alisema wamegundua waliofanyiwa vitendo vya udhalilishaji ni miongoni mwa watoto waliokosa malezi na maadili kutoka katika familia zao, hivyo kujiingiza katika vitendo viovu.

"Hawa wahanga (waathirika) tumewahoji kwa kina na kubaini kuwa ni miongoni mwa vijana ambao wazazi wao waliwashinda tokea wadogo, na kutelekezwa na baba yao hivyo kukosa malezi ya baba yao na kukosa maadili," alisema.

Kamanda Mchomvu alisema matukio hayo yametokea kwa sababu ya mmomonyoko wa maadili na kuwataka wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao katika kuwaamrisha mambo mema na kuwakata matendo maovu.

Pia alisema jeshi hilo linamshikilia Amour Suleiman Said (44) ambaye ni mtumishi wa umma kwa tuhuma za kumbaka mtoto wake wa kumlea (13) katika nyakati tofauti.

Katika hatua nyingine, Kamanda Mchomvu aliwaonya watu wanaotumia majina ya watu wengine na vyeo vya kipolisi kwa maslahi yao binafsi.

Alisema katika watuhumiwa 13 waliokamatwa na tuhuma za vitendo vya ulawiti, wako wanaojiita majina ya inspekta ambalo ni cheo cha kipolisi na mwingine kujiita jina la Zuchu ambalo ni jina la msanii.

"Ni kosa kisheria mtu kujiita jina ambalo si lake. Kwanza mtoto wa kiume vipi utajiita jina la Zuchu? Miongoni mwa tuliowakamata yuko ambaye umaarufu wake ni Zuchu na mwingine anajiita Inspekta hili ni kosa kisheria," alisema.

Watuhumiwa waliokamatwa kwa tuhuma hizo za vitendo hivyo vya udhalilishaji ni Ibrahim Saleh Mngwali, (29) mkaazi wa Sateen, Abrahman Saleh Rashid (22) maarufu Zuchu mkazi wa Raha Leo, Ali Abdallah Moh'd (27) mkazi wa Kisauni.

Wengine ni Yassir Abdallah Abdillah (17) mkazi wa Mwera, Twahir Salum Moh'd (25) mkazi wa Kisauni, Suleiman Juma Omar (22) mkazi wa Kisauni, Othman Moh'd Salum (49) mkazi wa Fuoni, Ali Haji Khamis (25) maarufu Inspekta Nyota Mbili, mkazi Kijichi.

Pia wamo Mudathir Jacob Simon (27) mkazi wa Magomeni Sogea, Ali Salim Abdallah (53) mkazi wa Shanghani, Mohamed Fuad Moh'd (21) mkazi Mkunazini.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, kwa mwezi wa Oktoba mwaka huu jumla ya matukio 199 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa, yakiwa na idadi ya waathirika 199 wa matukio hayo, ambapo waathirika wengi wakiwa ni watoto kwa asilimia 78.9, wanawake 16.1 na wanaume asilimia 5.0.

# Mashine maalum VVU yazinduliwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MASHINE maalum (ATM) ya kutolea huduma za vipimo vya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) ijulikanayo kwa jina la "Jipime" (HIV Self-Testing) imezinduliwa jijini hapa.

Lengo la huduma hiyo ni kuhamasisha wananchi kupima na kutambua afya zao ili kujilinda dhidi ya maambukizi mapya ya virusi hivyo.

Huduma hiyo ilizinduliwa jana na Mkurugenzi Mkazi wa Walter Reed Army Institute of Research (WRAIR) kutoka Ubalozi wa Marekani, Mark Breda, akiwa na mabinti na wananchi wengine waliohudhuria hafla ya uzinduzi wa mashine hiyo.

Katika hafla hiyo, Breda aliwataka vijana kuendelea kuchukua tahadhari kuepuka maambukizi mapya ya UKIMWI.

"Serikali ya Marekani kupitia WRAIR tumefanikiwa kufadhili upatikanaji wa mashine hizi zitakazo sambazwa hapa Mbeya na mikoa yote ya nyanda za juu kusini kupitia Shirika la HJFMRI, ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za VVU katika jamii," alisema Breda.

Awali, akizungumza kuhusu lengo la kuweka "ATM" hizo kwenye maeneo ya kutolea huduma za kijamii, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la HJF Medical Research International (HJFMRI), inayosambaza upatikanaji wa vipimo vya kujipima VVU vya Jipime, Sally Chalamila, alisema shirika lake limelenga kuwafikishia wananchi huduma za kupima VVU katika maeneo yao, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa vipimo vya Jipime na uhamasishaji wa matumizi ya kondomu.

"Mashine hizi zimeletwa kusaidia jitihada za serikali kufikia malengo ya kitaifa ya kufikia 95-95-95 ambapo katika 95 ya kwanza inataka kila Mtanzania kutambua afya yake kwa kupima VVU.

"Vipimo hivi vitapatikana bure na kila mwananchi ataweza kujipima VVU kupitia maelezo yaliyomo kwenye mashine na kipimo husika na endapo kipimo kitaonyesha kuwa na maambukizi anatakiwa kufika kwenye kituo cha afya ili kufanya kipimo cha uhakikisho" alisema Chalamila.

HJFMRI ni shirika la kimataifa lisilo la kiserikali linalotekeleza afua za matunzo na matibabu ya VVU kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia Timu za Usimamizi wa Afya za Mikoa na Halmashauri katika mikoa ya Mbeya, Songwe Rukwa na Katavi.

Katika mkoa wa Ruvuma, shirika linatekeleza afua moja tu ya tohara kwa wanaume ili kujikinga na maambukizi.

Chalamila alisema baadae mashine hizo zitawezeshwa kutoa huduma za dawa kinga maarufu kama (Pre-exposure prophylaxis (PrEP) na kwa mkoa wa Mbeya wanakusudia kuweka mashine kwenye maeneo yote ya starehe, vyuo vikuu, na maeneo yenye mikusanyiko mingi ya watu.

"Katika utekelezaji wetu wa afua hizi za UKIMWI hapa nchini, tumegundua kuwa kuna tatizo la maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 mpaka 24, ambapo hali ya maambukizi mapya kwa vijana hao ni asilimia 40 huku vijana wa kike ikiwa ni asilimia 80 na wakiume ikiwa ni asilimia 20, uwepo wa mashine hizi zitasaidia sana kundi hili kunufaika na njia za kujikinga na maambukizi mapya ya VVU," aliongeza.

Kwa mujibu wa Shirika la Ukimwi la Umoja wa Mataifa (UNAIDS), nchi zilizofanikiwa kufikia lengo la 95-95-95 ni Tanzania, Botswana, Eswatini, Rwanda na Zimbabwe.

Takwimu hizo zinamaana kuwa asilimia 95 ya watu wanaoishi na VVU wanajua hali zao za VVU, asilimia 95 ya watu wanaojua hali zao wanapata matibabu ya kurefusha maisha, na asilimia 95 ya watu wanaopata matibabu wamefubaza virusi hivyo, kwahiyo haiwezekani kusambaza.

# DAWASA yaja mfumo lipa maji kabla

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imeanza kufunga mita za kisasa za maji za kulipia ankara kabla ya matumizi.

Mpango huo ni sehemu ya kuepuka malimbikizo ya bili kutoka kwa wateja kama ilivyokuwa mwanzo pamoja na mfumo uliopo.

Mamlaka hiyo imeanza kufunga mita hizo kwenye vioski vya maji katika mji wa Chalinze mkoa wa Pwani kwa sehemu ya majaribio na baadaye kuendelea katika maeneo mengine ya kihuduma.

Ofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa DAWASA, Mhandisi Emmanuel Mwanyamaki, alisema jana kuwa uboreshaji wa mita hizo za kisasa unatekelezwa na wataalamu wa ndani wa mamlaka baada ya kubuni na kusanifu teknolojia hiyo iliyoasisiwa mapema mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema utaratibu wa kufunga mita za lipa kabla, ulianza Septemba, mwaka huu na sasa maboresho yanaendelea ili kuongeza ufanisi zaidi katika kutoa huduma ya maji.

"Mpaka sasa tumefanikiwa kufunga mita hizi kwenye maeneo mbalimbali vikiwamo vituo vya maji Mdaula, Chamakweza, Pingo na Mwindu na tunaendelea na maboresho, lakini tuko katika mchakato wa utekelezaji kwenye maeneo mengine," alisema Mwanyamaki.

"Kwa eneo la Chalinze, kuna vioski vya maji 550 na kwa kuanzia tumefunga kwenye zaidi ya vioski 10 na kazi hii itaendelea ili kukamilisha kwenye vioski vyote," alisema. Mwanyamaki aliongeza kuwa teknolojia hiyo ya mita za kulipa kabla ina manufaa mengi kwa wateja ikiwamo kupunguza upotevu wa maji na kuepusha upotevu wa fedha kwa wasimamizi wa vioski. Aliwaomba wasimamizi wa vituo vya maji Chalinze kuendelea kuwa mabalozi wazuri na waangalizi wazuri wa miundombinu hiyo ya maji ili idumu na kuendelea kutoa huduma kwa ufanisi mkubwa.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Mwidu, Hassan Mtemvu, alishukuru DAWASA kwa kuja na ubunifu mzuri wa mita za lipa kabla kwani italeta nafuu ya changamoto mbalimbali kwenye huduma ya maji.

"Ubunifu huu ni mzuri na utawawezesha wananchi kupata huduma bora na ya uhakika, na pia kupunguza upotevu wa maji mitaani," alieleza Mwenyekiti Mtemvu.

Msimamizi wa kituo cha maji Mdaula, Ester John, alisema amefurahishwa na mfumo huo wa mita za kulipa kabla kwa kuwa unawasaidia kuondokana na madeni kwa mamlaka.

Kuanza kwa matumizi ya mita za maji za kulipia kabla ni sehemu ya mapinduzi makubwa ya teknolojia yaliyotekelezwa na DAWASA na yatakayosaidia katika kupunguza upotevu wa maji mitaani, kupunguza gharama za ufuatiliaji madeni kwa sehemu za mbali.



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), wakisafisha miundombinu ya majitaka katika mitaa jijini Dar es Salaam jana, ili kuhakikisha inafanya kazi kwa ufanisi na kuepuka kuziba mara kwa mara kunakosababisha uchafuzi wa mazingira. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mlinzi kampuni binafsi auawa, watatu wajeruhiwa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MLINZI wa kampuni binafsi ya ulinzi ya Suma Guard mkoani Ruvuma, Boliva Mapunda (26), mkazi wa Kata ya Mateka, Manispaa ya Songea, ameuawa na watu wasiojulikana wanaodaiwa kuwa na mgogoro na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), huku watatu wakijeruhiwa.

Askari huyo alikuwa lindoni akiendelea na majukumu yake katika Hifadhi ya Misitu ya Safu ya Milima ya Livingstone iliyoko mpakani mwa wilaya za Nyasa na Mbinga, inayomilikiwa na TFS.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Kamishna Msaidizi (ACP) Marco Chilya, alisema tukio hilo lilitokea Novemba 20, mwaka huu, majira ya saa 2:00 asubuhi katika kijiji cha Mkali wilayani Nyasa.

Alisema zaidi ya wananchi 50 walivamia eneo la msitu huo na kuwakuta askari wakiwa lindoni kisha wakaanza kuwashambulia sehemu mbalimbali za miili kwa kutumia silaha za jadi kisha walinzi hao wakapoteza mwelekeo na mmoja kufariki dunia.

Kamanda Chilya aliwataja walijeruhiwa kuwa ni Yohana Komba, Kevini Mtitu na Daudi Kambanga.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni wananchi wa kijiji hicho kudai kuwa maeneo hayo ya hifadhi yanayomilikiwa na TFS ni yao ambayo yalichukuliwa na serikali bila kulipwa fidia.

Chilya alisema baada ya polisi kupata taarifa, walifanya msako na kuwakamata watu 40 wakiwa wamejificha kwenye mapango ya safu za Milima ya Livingstone jirani na vijiji vya Mkalia na Mkua wakiwa na silaha zao za jadi na gobole moja.

Kamanda Chilya alisema bado Jeshi la Polisi linaendelea na operesheni ya kubaini na kuwakamata waliohusika kwenye mauaji ya mlinzi na kuwajeruhi walinzi wengine ili wachukuliwe hatua za kisheria.

# Watumishi hospitali matatani kwa madai kuharibu ushahidi

**Na Moses Ng'wat,** MBOZI

WATUMISHI wanne wa Hospitali ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, wanashikiliwa na jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuharibu vielelezo vya ushahidi ili kumlinda Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Iporoto, Dk. Nyamosi Rioba (34).

Daktari huyo alikamatwa Julai 19, mwaka huu kwa tuhuma za wizi wa dawa na vifaa tiba.

Watumishi hao, kwa mujibu wa taarifa kutoka hospitalini hapo, wanadaiwa kuchezea vielelezo hivyo ambavyo ni dawa na vifaa tiba vilivyokamatawa na kuhifadhiwa, vikimhusu mganga mfawadhi huyo ambaye tayari amefikishwa mahakamani kwa madai ya wizi wa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. 1,066,120.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi (ACP) Theopista Mallya, alithibitisha kukamatwa kwa watumishi hao na kwamba wataunganishwa katika kesi ya wizi wa dawa na vifaa tiba ambayo inamkabili Dk. Rioba.

"Mtuhumiwa (Dk. Rioba ) alikamatwa na kuhojiwa kisha kufikishwa mahakamani Julai 31, 2023. Wakati upelelezi zaidi ukiendelea kuhusiana na tukio hilo, ilibainika kuwapo watumishi wengine wanne walioshiriki katika wizi huo, " alisema Kamanda Mallya.

Aliwataja watumishi hao ambao kwa sasa wanashikiliwa kuwa ni ni Muuguzi Mkuu Hospitali ya Wilaya ya Mbozi, Abdalbertha Haule, Mfamasia na Mteknolojia Dawa, Prosper Johnson, Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma, Stephano Kiluka, na Simoni Komba ambaye ni msimamizi wa huduma za maabara katika hospitali hiyo.

Julai 19, mwaka huu, Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe kwa ushirikiano na wananchi, lilimkamata Dk. Rioba kwa tuhuma za wizi wa dawa za binadamu, mali ya serikali na vifaa tiba katika zahanati hiyo ya kijiji.

HABARI KITAIFA

# Madalali kukusanya madeni kodi TBA

**Na Halfan Chussi**

KATIKA kupambana na wadaiwa sugu wa kodi ya pango katika nyumba za serikali, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) imesema inatarajia kutumia dalali wa mahakama ambaye ataanza kazi Desemba Mosi, mwaka huu, kukusanya madeni hayo.

Hatua hiyo, inaanzishwa baada ya deni hilo kufikia Sh. bilioni 7.8 huku wahusika wakuu wakiwa watumishi wa umma na taasisi mbalimbali za serikali.

Kuanza kwa mchakato huo kulitangazwa jana jijini Dar es Salaam na Mtendaji Mkuu wa TBA, Daud Kondoro, wakati akihamasisha wapangaji kulipa kodi kwa wakati.

Alisema dalali huyo aliyepatikana atazunguka nchi nzima kuwafikia wadaiwa wote na kuhakikisha wanalipa huku akisisitiza kuwa jambo hilo liko kwa mujibu wa sheria na kwamba atakayeshindwa kulipa hata kama ameondolewa kwa nguvu, atafunguliwa kesi ya madai.

Kondoro alisema kitendo cha wapangaji kushindwa kulipa kodi ya pango kwa wakati kinakwamisha juhudi za kuendeleza ukarabati na ujenzi wa nyumba zingine za watumishi.

"Moja ya hatua tutakazochukua ni kuwaondoa wadaiwa sugu kwa nguvu kupitia dalali wa mahakama aliyepewa zabuni hiyo kwa niaba ya TBA. Kwa sasa tayari kampuni ya udalali ya WINS Auction Mart, tumeshaikabidhi orodha ya wadaiwa sugu wote kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo ya kuwaondoa.

"Ninawataka wapangaji wetu wote kuhakikisha wanalipa madeni yao kwa wakati zikiwamo taasisi za umma baada ya kupokea namba za kumbukumbu za malipo ambazo hutumwa kwao kila mwezi kwa njia ya ujumbe mfupi," alisisitiza.

Aliwaarifu wapangaji kuanzia Desemba Mosi, mwaka huu, kuwa wataanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa Usimamizi wa Miliki za Serikali (GRMS) toleo la pili la mfumo mpya ambao utakuwa unatoza riba ya asilimia 20 kwa mpangaji atakayekaa zaidi ya miezi mitatu bila kulipa kodi ya pango.

Pia alisema tayari TBA imeshaanza kutumia vitasa janja, ili kudhibiti malimbikizo ya kodi ya pango akisisitiza mpango huo utaendelea kutekelezwa hadi kwenye nyumba zao za zamani.

Alizitaja taasisi zinazoongoza kwa madeni kuwa ni pamoja zile zilizoko Dodoma, Arusha, Mwanza na Mbeya na kwamba zinadaiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.4.




Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Jumanne Sagini (katikati) na Kamishna wa Polisi Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Suzan Kaganda, wakipokea mfano wa funguo kama ishara ya kupokea magari 43 kutoka Kampundi ya Ashok Layland yaliyokabidhiwa na Naibu Balozi wa India nchini, Manoj Varma (kulia), jijini Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa jeshi hilo. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Polisi yapokea magari 43 kukabili uhalifu

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi limepokea magari 43 kutoka Kampuni ya Ashok Leyland ya India ikiwa ni mwendelezo wa jitihada za serikali katika kuliwezesha jeshi hilo kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam katika hafla ya kupokea magari hayo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alisema magari hayo yametokana na mkataba wa masharti nafuu wa mwaka 2013 ulioingiwa kati ya Tanzania na India.

Sagini alisema mkataba huo ulikuwa na jumla ya magari 881 na baadhi ya magari yalishawasilishwa nchini na kubaki 20 na kwamba wako katika hatua za mwisho kupokea magari yaliyosalia.

"Tulikubaliana na Ashok Leyland kwamba ifikapo Januari, 2024 magari yaliyobaki ambayo ni 157 yatakuwa yameingia nchini. Lengo ni kuwezesha Jeshi la Polisi kutekeleza majukumu yao ipasavyo na haliwezi kutekeleza bila kuwa na vitendea kazi muhimu kama haya magari," alisema.

"Magari haya yana uwezo wa kwenda kilomita 200 kwa saa. Sasa kama mtu ataiba na gari lake akakimbia, tutamkamata tu muda si mrefu kwa sababu tuna magari yenye uwezo. Tumesisitiza madereva wapewe mafunzo ili wamudu kuendesha magari haya ipasavyo," alisema Sagini.

Pia alisisitiza kuwa katika matengenezo ya magari hayo, uwekwe mfumo ambao utahakikisha yanadumu kwa muda mrefu huku akiagiza Jeshi la Polisi kutenga bajeti ya matengenezo ya mara kwa mara ili magari hayo yadumu.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna wa Menejimenti ya Utawala na Rasilimali watu, Suzan Kaganda, alisema magari hayo yatatumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kuliwezesha jeshi hilo katika maboresho yanayoendelea ili kuongeza ufanisi wa kutoa huduma kwa wakati kwa wananchi.

Naye Naibu Balozi wa India nchini, Manoj Varma, alisema ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na India ni wa muda mrefu na umeendelea kuwa na manufaa makubwa kwa pande zote.

Alisema magari hayo yatalisaidia jeshi hilo kutimiza majukumu yake kwa urahisi na kwa wakati.

# Wahitimu wahimizwa ujenzi bweni wasichana

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAHITIMU wa Chuo Kikuu Mzumbe wamehimizwa kuchangia ujenzi wa bweni la mtoto wa kike katika Kampasi ya Mbeya ili kusaidia watoto wa jinsia hiyo kupata elimu inayostahili.

Rais Samia Suluhu Hassan alisema hayo jana kwenye hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, kwenye mkutano maalum wa 23 wa Baraza la Wahitimu wa Chuo Kikuu Mzumbe lililofanyika chuoni hapo, nje kidogo ya mji wa Morogoro.

Alisema akiwa mmoja wa wahitimu wa chuo hicho, aliyehitimu mwaka 1986, ameona ujenzi wa bweni la mtoto wa kike kuwa ni sehemu ya kuhimiza na kumsomesha mtoto wa kike kwa manufaa ya watu wote.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, aliwataka wahitimu wa chuo hicho kuwa mstari wa mbele katika kuchangia ujenzi wa bweni hilo la wasichana Mbeya kwa maendeleo ya chuo hicho.

Prof. Ole Gabriel ambaye pia ni mmoja wa wahitimu wa chuo hicho, aliwasihi wahitimu kuwa mabalozi wazuri wa kukitangaza chuo popote wanapokuwa.

Rais wa Baraza la Wahitimu wa Chuo hicho, CPA Ludovick Utouh, alisema kuanzishwa kwa baraza ni mkakati wa kuboresha nidhamu kwa wanachuo na kutaka chuo kwenda mbali zaidi kwa maendeleo.

CPA Utouh ambaye pia ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, alisema kupitia baraza hilo, wameshajenga bweni la Maria Nyerere lililoko kampasi ya Mzumbe. Aliwataka wahitimu kujitoa katika kuchangia ujenzi wa bweni jipya la Mbeya.

Awali , Kaimu Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Prof. William Mwegoha, alisema Sh. bilioni 6.65 zimetumika katika kukamilisha ujenzi wa mabweni ya wanafunzi yatakayosaidia wanavyuo katika eneo jipya la Maekani lililoko kampasi ya Morogoro.

Prof. Mwegoha alisema ujenzi huo ulikamilika mwaka 2021 na mabweni hayo yameanza kutumika tangu kuanza kwa mwaka huu wa masomo wa 2023/24.

Pia, alisema fedha hizo zimetokana na mapato ndani pamoja na serikali kuu huku Sh. milioni 924 zikitengwa kwa ajili ya kuimarisha miundombinu iliyoko kwenye eneo jipya ukiwamo ujenzi wa barabara za ndani.

**Alisema akiwa mmoja wa wahitimu wa chuo hicho, aliyehitimu mwaka 1986, ameona ujenzi wa bweni la mtoto wa kike kuwa ni sehemu ya kuhimiza na kumsomesha mtoto wa kike kwa manufaa ya watu wote.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wenye sifa ya kujiandikisha Daftari la Mpigakura fursa hiyo

**WAKATI** uchaguzi mkuu ukikaribia kufanyika nchini, Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), zimeanza maandalizi ya uandikishaji wa Daftari la Mpigakura.

Hii ni hatua muhimu katika kutoa haki kwa kila Mtanzania kupata fursa ya kumchagua kiongozi anayemtamani kumwongoza.

Daftari la Mpigakura hutoa fursa kwa Watanzania ambao wakati likianzishwa kuna ambao walikuwa hawajafikia umri wa kupiga kura ambao ni miaka 18 na sasa wamefikia umri huo ili nao wapate haki yao ya kupiga kura.

Vile vile, daftari hili husaidia kuboresha taarifa za watu ambao wamehama makazi yao ya awali na kuhamia kwingine ili waweze kutambulika wakati wa kupiga kura.

Kuna taarifa pia za watu ambao walijiandikisha kwenye daftari hilo, lakini kwa sasa wameshatangulia mbele ya haki.

Utaratibu huu husaidia kuwabaini pia wadanganyifu na kuwaondoa kwenye orodha ya daftari hilo ili unapofika wakati wa kupiga kura kusijitokeze malalamiko na kuharibu dhana nzima ya kuondoa sintofahamu.

Kwa upande wa Tanzania Visiwani, kazi ya uandikishaji inaanzia Pemba na Wazanzibari wenye sifa, wameombwa kujitokeza kuandikishwa katika daftari la kudumu la wapigakura.

Tayari Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), imetoa taarifa kwa wananchi kuandikisha wapigakura wapya, kuanzia mwezi Desemba ili kutimiza matakwa ya sheria kama Katiba ya Zanzibar inavyoelekeza, kuanzisha daftari la kudumu la wapigakura na kuweka utaratibu wa kurekebisha taarifa zao wapigakura katika daftari hilo.

Ibara ya 8 (A) ya Katiba ya Zanzibar inaeleza kuwa mamlaka ya kuendesha nchi ni wananchi wenyewe, ambapo nguvu na mamlaka inatokana na wananchi wenywe."

Ili kufikia malengo hayo lazima wananchi wajitokeze kujiandisha kupata nafasi ya kupiga kura, kutimiza matakwa yao ya kisheria, kwa kuwa wasipojiandisha watakosa haki ya kuwachagua viongozi wanaowataka.

Wazanzibari wote wenye vyama na wasio na vyama wametakiwa kujitokeza kujiandisha katika daftari hilo na hata asiye na chama ana haki ya kupiga kura kama atajiandikisha mapema.

Tume ya uchaguzi inajukumu pia la kuangalia na kuondoa kasoro ndogo ndogo ili kila mmoja apate haki yake.

Masheha pia wametakiwa kuzingatia sheria ya uchaguzi kwa kutowazuia watu kujiandikisha, kwa sababu wenye mamlaka ya kufanya hivyo ni Tume ya Uchaguzi kwa vigezo vilivyowekwa kisheria.


Pia wananchi ambao hawana sifa ya kujiandikisha wahakikishe hawafiki katika vituo vya kujiandisha, ili kuondoa fujo ambazo hazina msingi.

Kwa upande wa Tanzania Bara Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inatarajia kuanza majaribio ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura katika mikoa miwili ya Tabora na Mara ambayo imechaguliwa kwa ajili ya kufanya majaribio hayo lengo likiwa kupima utayari wa mifumo na vifaa vya uboreshaji wa daftari hilo.

Lengo lingine la uboreshaji wa taarifa hizo ni kuandikisha kila raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi na atakayetimiza umri huo kabla au ifikapo tarehe ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Kundi lingine litakalohusika kwenye uboreshaji huo ni wapigakura wanaoboresha taarifa zao ambao wamehama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda eneo lingine, waliopoteza au kuharibikiwa na kadi, wanaorekebisha taarifa zao na kuondoa wapigakura waliopoteza sifa za kuwamo katika daftari.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Mary Seme

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ifikie zama makondakta nao waheshimiwe kwa hadhi zao

**IMEKUWA** jambo la kawaida na lililozoeleka kwa makondakta wa daladala katika maeneo mbalimbali ya hapa nchini kutokuheshimika, huku baadhi ya watu wakitumia kauli chafu dhidi ya hao makondakta.

Jambo ambalo linawadhalilisha makondakta hawa na kuwafanya wajisikie wanyonge kulingana na kauli mbaya zitolewazo na baadhi ya abiria wasio wastaarabu.

Kazi ya ukondakta ni kazi kama zilivyo kazi nyingine za maofisini, tofauti yake ni katika mazingira wanayofanya kazi.

Unakuta kondakta anadharaulika kutokana na mavazi yake anayovaa, jinsi alivyo pengine na muonekano wake wa nje ulivyo. Si jambo zuri kuwaudhi na kutumia kauli zenye kashfa mbaya dhidi ya wahasibu hawa wa fedha katika daladala.

Unaweza kukuta katika gari kondakta anajaribu kuwapanga vizuri ili wote waenee, lakini baadhi ya abiria wakaidi wanakuwa wagumu kuelewa na kuishia kuwatolea kauli chafu, hata kuwatukana, jambo ambalo limekuwa ni kero kwa abiria wengine pindi wanapoona hayo yanatokea.

Tukumbuke kuwa makondakta hawa ni kaka, baba, dada, shangazi na mjomba kwa watu wengine, hivyo tusiwanyanyase na kufanya maisha yao kuwa magumu.

Pia, tukumbuke bila wao hakuna kinachoweza kuendelea kwenye vyombo hivi vya usafiri hivyo ni muhimu kutambua nafasi yao.

Baadhi ya watu hudai kuwa, makondakta wa daladala ni wakorofi, lakini ukweli ni kutokana na mazingira ya kazi zao ya kukutana na abiria wakorofi na wenye kuudhi, mwingine kwa makusudi tu hataki kutoa nauli au anatoa nauli pungufu bila makubaliano je unatarajia nini kutoka kwa kondakta ambaye kipato chake ni kidogo?

Je akija mwingine na kweli akawa na nauli pungufu au amepoteza nauli ataeleweka? Tuwape thamani makondakta hawa, ili kutokuwaathiri kisaikolojia na matokeo yake wanakuwa na hasira kila wakati, lakini kumbe chanzo chake ni tabia za abiria.

**Hali kama hiyo inapotokea inamfanya kondakta kuhisi kudharauliwa na hivyo ili kurejesha heshima yake hana budi kuwa mkali kama pilipili kulazimisha kulipwa haki yake ya nauli, mbaya zaidi ni pale abiria wengine wanaposhindwa kusimama upande wa haki na kuegemea upande wa abiria mwenzao kana kwamba alichokifanya ni kitu sahihi.**

Sehemu yoyote ukitaka kuhudumiwa vizuri ni vyema wewe mwenyewe pia ukaanza vizuri, mathalan kuwa na lugha nzuri kwa mtoa huduma husika.

Vinginevyo wewe ukianza vibaya, tambua kuwa huwezi kuhudumiwa vizuri. Siku moja nilishuhudia abiria amepanda gari mpaka mwisho wa kituo na badala ya kutoa nauli akadai ya kwamba eti amepelekwa kituo tofauti hivyo hawezi kutoa nauli.

Baadhi ya abiria tulibaki tukimshangaa, kwamba iwapo hakujua kusoma inapoishia gari, ni kwanini hakufanya ustaarabu angalau wa kuuliza kwa abiria wengine?

Kwa muonekano tu, alionekana si mtu ambaye hajui kusoma na kuandika, pia hana shida ya kusikia, hata useme hakusikia vituo vinapotangazwa kila daladala inaposimama, hivyo ashindwe kugundua kuwa amepanda daladala tofauti na anapoelekea hata afike kituo cha mwisho ndipo agundue hilo.

Hali kama hiyo inapotokea inamfanya kondakta kuhisi kudharauliwa na hivyo ili kurejesha heshima yake hana budi kuwa mkali kama pilipili kulazimisha kulipwa haki yake ya nauli, mbaya zaidi ni pale abiria wengine wanaposhindwa kusimama upande wa haki na kuegemea upande wa abiria mwenzao kana kwamba alichokifanya ni kitu sahihi.

Ila niwape ndugu zangu hao angalizo, kwamba heshima mbele ya jumuiya, ambako kuna mema na maasi, kuna vigezo na masharti yake, kwamba vinatengezwa, ili kujihakikishia heshima.

Pengine inaweza ikaibua swali, kwa vipi? Makondakta watakapovaa kwa unadhifu na usafi, huku wakiambatanisha vigezo vya nidhamu kazini, hapana shaka watajihakikishia hilo ninalowapigia upatu.

HABARI KITAIFA

# UN Women kuwezesha wanawake, wasichana

**Na Faustine Feliciane**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Wanawake (UN Women), limezindua mpango wa kusaidia na kuwezesha wasichana na wanawake wa Kitanzania kupata ujuzi wa sayansi, teknolojia, uhandisi na Hisabati kwa mfumo wa kidigitali.

UN Women wataendesha mpango huo kwa kushirikiana na kampuni ya huduma za simu ya Tigo, wakiwezesha wasichana wenye umri kuanzia miaka 17 hadi 25 kuchukua masomo na taaluma katika sekta ya Habari, Teknolojia na Mawasiliano (TEHAMA).

Wakati wa kutia saini mkataba wa awali wa makubaliano kati ya taasisi hizo juzi, Mwakilishi Mkazi wa UN Women nchini, Hodan Addou, alisema ushirikiano huo unalenga kuunga mkono juhudi za serikali kuongeza usawa wa kijinsia na kuwapa fursa wanawake kuchangia uchumi wa kidigitali.

Addou alisema takwimu zinaonesha kuwa asilimia 90 ya kazi zijazo ulimwenguni zinahitaji ujuzi wa TEHAMA.

"Lakini uandikishaji katika masomo ya sayansi unaonesha pengo kubwa la kijinsia na wasichana wachache kuliko wavulana wanaoshiriki, wanawake wana uwakilishi mdogo katika taaluma za sayansi na uhandisi, mpango huu tunaoshirikiana na Tigo utasaidia kuondoa pengo lililopo sasa," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Kamal Okba, alisema mpango huo utasaidia kutomwacha mwanamke nyuma kwenye masuala ya TEHAMA na digitali.

Alisema Tigo kwa kushirikiana na UN Women wamedhamiria kuziba pengo la kijinsia katika sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati.




Wanafunzi waliohudhuria kampeni ya kutokomeza malaria ya Barrick Bulyanhulu katika Kijiji cha Lwakabanga, wakiwa pamoja na maofisa wa kampuni hiyo, baada ya kukabidhiwa vyandarua vyenye dawa vya kuwakinga dhidi ya ugonjwa huo, katika kampeni inayoendelea kwa kipindi cha wiki moja wilayani Msalala, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfumo mpya utendaji kazi utumishi mwarobaini wasiotimiza majukumu

**Na Lusungu Helela,** IRINGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amesema mfumo mpya wa usimamizi wa utendaji kazi wa mtumishi na taasisi (PEPMIS & PIPMIS) ni mwarobaini kwa watumishi wasiotekeleza wajibu wao.

Kikwete alisema hayo juzi mjini hapa wakati akifungua mafunzo hayo yanayoenda sambamba na mafunzo ya mfumo wa tathmini ya mahitaji ya rasilimali watu utakaowezesha kubainisha mahitaji katika taasisi husika.

Akizungumza katika ufunguzi huo na watumishi wa mamlaka za serikali za mitaa zilizoko mkoani hapa pamoja na taasisi na mashirika ya umma, Kikwete alisema mifumo hiyo imelenga kuboresha utendaji kazi unaojali matokeo na tija katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Tumetuma wataalamu nchi nzima kwa ajili ya kujenga uelewa wa namna ya kutumia mifumo hiyo ya kidijitali ambayo tunaamini itasaidia watumishi wa umma kuwahudumia wananchi kwa viwango vya juu," alisema.

Kikwete alisema mwanzo serikali ilikuwa ikitumia mfumo wa wazi wa mapitio na upimaji wa utendaji kazi (OPRAS) kusimamia utendaji kwa watumishi wa umma lakini kutokana na changamoto zake, imeamua kuja na mfumo mpya ambao utajibu changamoto za mfumo huo wa zamani.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, aliishukuru Ofisi ya Rais Utumishi kwa kufika Iringa kutoa mafunzo ya namna ya kutumia mifumo hiyo ya kidijitali kwa ajili ya kupima utendaji kazi wa watumishi. Aliihakikishia ofisi hiyo kupata ushirikiano wa kutosha.

Timu ya wataalamu kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi ikiongozwa na Mkurugenzi wa Mikataba ya Utendaji Kazi, Zainab Kutengezah, iko mkoani Iringa kutoa mafunzo kwa watumishi kuhusu namna bora ya kutumia mifumo hiyo.

# Meli tatu kukarabatiwa kwa bilioni 48/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Dar es Salaam Merchant Group (DMG) imeahidi kukarabati kwa viwango na kwa wakati meli ya abiria na mizigo MV. Liemba iliyoko mkoani Kigoma (Ziwa Tanganyika), MV. Ukerewe pamoja na meli ya MT. Nyangumi zinazofanya kazi Ziwa Victoria.

Jijini Mwanza baada ya kutia saini mikataba hiyo mitatu ya ukarabati wa meli hizo na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) yenye thamani ya zaidi bilioni 48, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Dar es Salaam Merchant Group (DMG), Rayton Kwembe alisema:

"Tunaaidi ukarabati uliotukuka na wenye viwango ambapo kwenye utekelezaji huu tunafanya kwa ushirikiano na Kampuni ya M/S Brodosplit JSC ya Croatia kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 48."

Mkurugenzi huyo alisema ukarabati wa meli kongwe ya abiria na mizigo MV. Liemba utagharimu Sh. bilioni 32 wakati ukarabati wa MV. Ukerewe utafanywa kwa Sh. bilioni sita huku ukarabati wa meli ya MT. Nyangumi ukitarajiwa kugharimu Sh. bilioni nane.

Kwembe alishukuru serikali kwa kuendelea kuwaamini na kuahidi kamwe hawatawaangusha katika utekelezaji wa miradi hiyo.

"Ili kutekeleza vyema miradi ya ujenzi wa meli na matengenezo yake, DMG ilianzisha idara ya kushughulikia mambo hayo mwanzoni mwaka 2017 kwa nia ya kutatua changamoto zinazoikabili sekta hii iliyo katika uchumi wa bluu," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL, Eric Hamissi alisema serikali imeamua kuwekeza katika ukarabati wa meli hizo kutokana na uimara wake na kuokoa gharama ya kujenga au kutengeneza meli mpya.

"Kuna watu walikuwa wananiuliza kwanini serikali inafanya ukarabati wa meli hii sasa? Ni wajibu kwamba mbali na meli hizi kuwa na miaka mingi lakini gharama za kutengeneza meli mpya kama hizi moja ni zaidi ya Sh. bilioni 120, lakini pia baada ya wataalamu kuchunguza meli zilizopo tulibaini bado vyuma vyake vina ubora mkubwa na havina uchakavu, ndio maana serikali ikaamua kuwekeza," alisema Hamissi.

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini wa mikataba mitatu ya ukarabati wa meli uliofanyika katika Bandari ya Kusini jijini Mwanza, Naibu Waziri wa Wizara ya Uchukuzi, David Kihenzile alitaka ukarabati huo kuzingatia muda wa mkataba.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED





Viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wakiwa katika moja ya mikutano yao hivi karibuni **PICHA: MAKTABA**

# Wakuu nchi Afrika Mashariki waanza mkutano Arusha

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

VIONGOZI wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wanaanza mkutano wa siku mbili jijini Arusha leo, ambao awali ulikuwa ufanyike nchini Burundi.

Kura imeangukia Tanzania ambayo inang'ara katika masuala ya diplomasia za kimataifa.

Mkutano huo wa viongozi wakuu wa nchi hizo utakuwa chini ya mwenyeji wao Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, William Ruto wa Kenya, Paul Kagame wa Rwanda na Evariste Ndayishimiye wa Burundi. Pamoja nao ni Felix Tshisekedi wa DRC, Salva Kiir wa Sudan Kusini na Yoweri Museveni wa Uganda.

Kufanyika kwa mkutano huo jijini Arusha ni heshima nyingine inayopewa Tanzania ambayo inasifika kwenye masuala ya kidiplomasia, lakini pia ikiwa ni kisiwa cha amani tangu Uhuru 1961.

Ni wazi kuwa kwa Afrika Mashariki, Tanzania inaendelea kuwa na raia wanaoishi kwa amani na kudumisha hisia za umoja na utaifa mmoja bila kuwa na mgawanyiko wa udini, rangi au ukabila licha ya kwamba kuna makabila zaidi ya 130.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, uenyekiti huo wa EAC ni wadhifa wa mzunguko ambao unashikiliwa na kila nchi mwanachama kwa muhula wa mwaka mmoja na rais wa taifa ambalo mkutano hufanyika ndiye anakuwa mwenyekiti na kwa sasa ni Burundi.

Juhudi zinazofanywa na Rais Samia kuijenga nchi kwa serikali kuwa sikivu, kupokea maoni mbalimbali ikiwamo ya kuboresha mazingira mazuri ya kibiashara na uwekezaji, zimefungua fursa nyingi za wageni kuitembelea Tanzania.

Katika mkutano huo wa 23 wa Wakuu wa Nchi za EAC, mambo mengi yatajadiliwa ikiwa ni pamoja na suala la amani hasa migogoro ya vita na uasi nchini DRC, ambako waasi wa M23 na vikundi mbalimbali vya kiasi kama Maimai kutishia amani Mashariki mwa Congo.

Kadhalika, Sudan Kusin ambako kuna mgogoro wa ndani baina ya viongozi wakuu wa nchi ni moja ya ajenda zitakazofikishwa mezani. Kadhalika mengine yatakayozungumzwa na wakuu hao ambao Mwenyekiti wa EAC safari hii ni Jenerali Evariste Ndayishimiye ni mabadiliko ya tabianchi.

Viongozi wa EAC wanajadili kadhia za mabadiliko ya tabianchi kipindi hiki zikiwa zimesalia siku saba kabla ya kuanza mkutano wa kilele wa mazingira duniani COP28, unaofanyika Dubai, kuanzia Novemba 30.

Mabadiliko ya hali ya hewa yamesababisha changamoto mbalimbali kwa Afrika Mashariki ikiwamo njaa, ukame na nzige wanaoongeza uhaba wa chakula na ugumu wa maisha.

Aidha, mafuriko, vifo, uharibifu wa miundombinu hasa nchini DRC ni mambo yanayohitaji nguvu za pamoja kujikwamua makubaliano pengine yakianzia katika mkutano huo.

Vilevile, viongozi wa EAC wanatarajiwa kupokea ripoti ya uanachama mpya wa Somalia kwenye umoja huo, mkutano wa 23 wa kawaida mjini Arusha, ukitegemewa kutoa baraka za kuidhinisha mwanachama mpya.

Viongozi hao wanatarajiwa kujadili Somalia inayoomba kuwa mwanachama wao mpya, ambao pia watafahamishwa hatua za mwisho za mchakato wake wa kujiunga na EAC huku kukiwa na uwezekano wa kuikaribisha rasmi mwaka huu.

Kuikaribisha Somalia kuliidhinishwa kwenye mkutano wa 22 wa kawaida wa wakuu wa nchi za EAC ambao ulitoa maelekezo kwa baraza lake kufuatilia zoezi la uhakiki kwa mujibu wa taratibu za EAC za uandikishaji wa wanachama wapya.

Katika mkutano huo mwenyeji Tanzania ambaye ni lango la kiuchumi ana fursa ya kujitangaza kwa wanachama wake akiwamo Sudan Kusini, DRC, Rwanda, Burundi na Uganda hasa kwenye usafirishaji na uchukuzi wa shehena.

Ikumbukwe kuwa kitu ambacho nchi hii inajivunia na kukigeuza kuwa fursa kwa kila mwana EAC ni kuwa lango la uchukuzi hasa Bandari ya Dar es Salaam ambayo sasa imepata nguvu mpya baada ya ujenzi wa reli ya kisasa ya mwendo kasi (SGR) na kukamilika kwa bandari kavu ya Kwala.

Hivyo kijiografia Tanzania iko katika eneo ambalo ni lango kwa nchi nyingi za EAC, lakini pia za Kusini mwa Afrika ikiwamo Malawi, Zambia na hata Zimbabwe.

**Juhudi zinazofanywa na Rais Samia kuijenga nchi kwa serikali kuwa sikivu, kupokea maoni mbalimbali ikiwamo ya kuboresha mazingira mazuri ya kibiashara na uwekezaji, zimefungua fursa nyingi za wageni kuitembelea Tanzania.**

Utayari wa bandari kavu ya Kwala iliyopo mkoani Pwani, ambayo imekamilika na kuhudumia shehena inayopokelewa kwenye Bandari ya Dar es Salaam na kuielekeza mikoa mbalimbali na mataifa jirani, ni fursa tosha ya kibiashara.

Bandari ya Kwala itapunguza msongamano wa mizigo na magari makubwa katika Bandari ya Dar es Salaam kwa vile ina uwezo wa kuhifadhi makasha au makontena ya mataifa wanachama wa EAC kama Burundi, Rwanda, DRC Congo, Uganda, Sudan Kusini, lakini pia Zambia na Malawi.

Ujenzi wa bandari ya kavu ya Kwala utapunguza kwa kiasi kikubwa foleni ya malori Bandari Dar es Salaam na kurahisisha utendaji wa bandari hiyo kwa kuwa mizigo itashushwa kwenye meli na kupelekwa bandari hiyo.

Ikumbukwe kuwa usafirishaji kwa ufanisi wa shehena na watu ni masuala muhimu katika ujenzi wa uchumi imara na kuendeleza mtangamano miongoni mwa nchi wanachama hasa ambao wanategemea Bandari ya Dar es Salaam.

# Makada 20 wajitosa kumrithi Zelothe CCM

**Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAFASI ya Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha imevutia wengi, hadi jana mchana, makada 20 walikuwa wamejitokeza kuchukua fomu.

Wakati makada hao wakipigana vikumbo kutaka kumrithi aliyekuwa Mwenyekiti wake, marehemu Zelothe Steven, Katibu wa CCM mkoani Arusha, Musa Matoroka, ameonya wanaofanya kampeni za siri ili kutengeneza mazingira ya ushawishi na kukubalika kwao.

Jana akizungumzia mchakato huo wa kujaza nafasi hiyo iliyoachwa wazi na Zelothe, Kamishna wa zamani wa Jeshi la Polisi nchini (CP) aliyefariki dunia Oktoba 26 mwaka huu, Matoroka alisema makada hao hawaruhusiwi kufanya kampeni hadi hapo Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, itakapoketi na kuteua wagombea.

Kwa mujibu wa Matoroka, pazia la uchukuaji fomu za kujaza nafasi hiyo lilianza Novemba 21 na litafungwa jioni ya Novemba 23, mwaka huu.

"CCM ina intelijensia kubwa, na hivi sasa inaendelea kufuatilia mienendo yote ya wagombea wanaochukua fomu na ikithibitika kuwa kuna mgombea anafanya kampeni kwa namna yoyote ile, hilo hatua kali za kikanuni zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kuengua jina lake.

"Marufuku kwa wagombea wote wanaochukua fomu kuanza kufanya kampeni za kuomba kura na kufanya kampeni za kuwapaka matope wagombea wenzao kwa wajumbe wanaotakiwa kupiga kura.

"Hiyo ni kwa sababu bado ni mapema mno na watambue kwamba tunawafuatilia kwa karibu na ikithibitika kuwa kuna wagombea wameanza kufanya kampeni, majina yao yataenguliwa mara moja," alionya.

Kuhusu gharama za kuchukua fomu, Matoroka alisema hakuna gharama zozote. Fomu zinatolewa bila malipo.

Wanaotajwa kupigana vikumbo kutaka kumrithi Zelothe ni baadhi ya vigogo wastaafu serikalini, wakiwamo wakuu wa mikoa, 'kigogo' toka Halmashauri Kuu ya CCM (NEC) na makada wengine wa chama hicho wasio na majina makubwa kisiasa.




Ofisa Mikopo wa Mfuko wa SELF, Mbwana Msangule (katikati), akitoa elimu ya masuala ya fedha kwa wananchi waliotembelea banda lao katika maonyesho ya tatu ya Wiki ya Huduma za Kifedha kitaifa, kwenye viwanja vya Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# AUABC yaipongeza Tanzania mapambano dhidi ya rushwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BODI ya Kupambana na Rushwa ya Umoja wa Afrika (AUABC) imeipongeza Tanzania kwa jitihada zake za kuzuia rushwa na utoaji elimu kwa watoto shuleni.

Mwenyekiti wa bodi hiyo, Seymabou Diakhate, aliipa kongole Serikali ya Tanzania jana jijini Arusha alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kikao cha bodi hiyo kinachoendelea.

Mbali na mambo mengine, kikao hicho kinachojadili namna nchi za Afrika zinavyopambana na masuala ya rushwa. Kilianza Novemba 20 na kitahitimishwa Novemba 28 mwaka huu.

Alisema Tanzania imepiga hatua ya kupambana na rushwa kwa uanzishwaji klabu za mapambano ya rushwa kwenye shule, pia hata mahakamani kesi zinasikilizwa ipasavyo ikiwamo wale wanaotumia miradi kujipatia fedha isivyo halali.

"Bodi inaipongeza Tanzania kwa kupiga hatua kubwa katika mapambano ya rushwa kwa sababu wanaklabu za watoto shuleni na hata kesi za rushwa zinafikishwa mahakamani," alisema.

Mwenyekiti huyo pia alisema vita dhidi ya rushwa haiwezi kufanikiwa kama rasilimali zilizoibwa Afrika, hazitarejeshwa na hilo litafanikiwa kwa nchi hizo kuungana kupigania fedha zilizoibwa zirejeshwe.

"Lazima nchi za Afrika ziungane kuhakikisha rasilimali zilizoibwa zinarejeshwa, kwa kuwa kuna mbinu nyingi zinazotumika katika kutekeleza uhalifu wa wizi wa fedha kupeleka nchi za nje," alisema.

Kiongozi huyo alisema walitegemea fedha zilizofichwa Ulaya na baadhi ya viongozi baada ya kupinduliwa yale mataifa ya Ulaya yangezirudisha, lakini hakuna kilichorejeshwa mpaka sasa na ipo mifano mingi katika hilo.

Diakhate alisisitiza ni vyema mataifa ya Afrika yakatumia AUABC kubadilishana uzoefu katika kukabiliana na rushwa, ikiwamo mikataba ya uwekezaji kwenye rasilimali wanayoingia na kampuni kubwa zinazowekeza Afrika ili wanufaike na uwekezaji huo.

# Wabuni teknolojia ya kuzuia mboga, matunda kuharibika

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

KITUO cha Dunia cha Mboga (WVC) kimebuni teknolojia ya kisasa ya kuziongezea maisha bidhaa zinazotokana na mboga, matunda na viungo, hata kutoharibika na kupoteza ubora katika kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja zikiwa sokoni.

Jana Mtafiti Mwandamizi wa WVC (World Vegetable Centre), Omari Mbwambo, alisema upotevu wa mazao hayo nchini kwa sasa baada ya kuvunwa ni asilimia 50.

Alikuwa akizungumza na timu ya waandishi wa habari za kilimo waliotembelea mashamba ya kuzalishia mbegu za aina mbalimbali yanayosimamiwa na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti na Uendelezaji wa Kilimo cha Mboga Kanda ya Mashariki na Kusini Mwa Afrika kuelekea Jubilee ya miaka 50.

"Hizi mboga ambazo ni perishable (zile ambazo haziwezi kukaa kwa muda mrefu), nyingi zina kiwango kikubwa cha maji. Ili kuzuia huo upotevu kuna teknolojia mbalimbali kama tannel solar drier, ambayo hukausha mazao haya kwa kutumia nishati ya jua.

"Faida ya tannel solar drier ni kuziongezea maisha hizi bidhaa zinazotokana na mboga. Inapunguza maji, na mboga inaweza kukaa kwa muda mrefu zaidi. Inaweza kukaa hadi mwaka mmoja baada ya kuzikausha. Joto lake la kukaushia ni mpaka kufikia nyuzi joto 70," alisema.

Kituo hicho pia kimefanikiwa kuja na aina 360 za mbegu za mchicha, ambazo zinawapa wakulima fursa ya kuchagua, kulingana na mahitaji.

Kwa mujibu wa Mbwambo, ambaye pia ni Meneja wa Mashamba ya WVC, katika utafiti wao, zao la mchicha limepewa kipaumbele zaidi kwa kuwa ni asili ya Afrika, hasa kutokana na kulimwa kwa muda mrefu.

Mwanasayansi na Mtafiti wa Mbegu za Asili za Mboga wa WVC, Dk. Sognigbe, alisema taasisi hiyo ni ufunguo wa mkusanyiko wa mbegu za asili za Afrika, inayolenga kukusanya, kuzifanyia utafiti, kuziboresha na kuzihifadhi kwa ajili ya kilimo na lishe, pia mahususi kwa ajili ya vizazi vijavyo.

"Tumekusanya mbegu zaidi ya 6,000 za mboga na katika hizo, tumeweza kuzifanyia utafiti na kuziboresha. Kutokana na mbegu hizo, sasa tumeweza kuzalisha mbegu mpya zaidi ya 100 ambazo ni rafiki, zikiwamo za mchicha, mnavu na nyinginezo ambazo ni tunazoita mbegu za asili za Afrika," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. N'Danikou, WVC inapokea mbegu kutoka kwa wakulima wa maeneo mbalimbali ya Tanzania, Uganda, Kenya, Madagascar, Benin na Senegal.

"Nchi nyingine zinakuja katika kifungashio kidogo sana, ambapo tunachokifanya ni kuziendeleza kwa kuzizalisha katika mashamba yetu ili kuwa na mbegu ya kutosha, lakini pia tunazijaribu ili kupata mbegu zenye ubora.

"Kingine tunachokifanya katika GeenBank (Benki ya Vinasaba vya Mbegu) ni kusambaza, kwa sababu benki hii si makumbusho, useme watu watakuja kuangalia na kuondoka.

"Mbegu ni lazima itumike kwa ajili ya uzalishaji. Kwahiyo, tunasambaza mbegu kupitia miradi ya kimaendeleo, ambayo inawafanya wakulima kuzifikia mbegu hizi na kuzitumia katika bustani za nyumbani, za shule na maeneo mengine," alisema.





# Majaribio uboreshaji wa daftari la kudumu kufanyika Tabora, Mara

**Na Halima Ikunji,** TABORA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), inatarajia kuanza majaribio ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura katika mikoa miwili ya Tabora na Mara ambayo imechaguliwa kwa ajili ya kufanya majaribio hayo kupima utayari wa mifumo na vifaa vya uboreshaji daftari.

Mjumbe wa NEC, Balozi Omar Ramadhan Mapuri, alisema hayo wakati wa ufunguzi wa mkutano wa Tume na wadau wa uchaguzi uliofanyika juzi mkoani hapa na kuwataka wakazi wa maeneo yaliyochaguliwa kushiriki kikamilifu ili kufanikisha hatua hiyo.

Balozi Mapuri alisema majaribio hayo yataanza Novemba 24 hadi 30 katika Kata za Ng'ambo Halmashauri ya Manispaa ya Tabora mkoani hapa na Ikoma iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, mkoani Mara.

"Uboreshaji wa majaribio kwenye kata hizo utafanyika katika vituo 16 vya kuandikisha wapigakura ambako vituo 10 vipo katika Kata ya Ng'ambo na vingine sita katika Kata ya Ikoma ambavyo vitafunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni," alisema Balozi Mapuri.

Uboreshaji wa taarifa hizo ni kuandikisha kila raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi na atakayetimiza umri huo kabla au ifikapo tarehe ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Vilevile, alitaja kundi lingine litakalohusika kwenye uboreshaji huo kuwa ni wapigakura wanaoboresha taarifa zao ambao wamehama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda lingine, waliopoteza au kuharibikiwa na kadi, wanaorekebisha taarifa zao na kuondoa wapigakura waliopoteza sifa za kuwamo katika daftari.

**"Uboreshaji wa majaribio kwenye kata hizo utafanyika katika vituo 16 vya kuandikisha wapigakura ambako vituo 10 vipo katika Kata ya Ng'ambo na vingine sita katika Kata ya Ikoma ambavyo vitafunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni," alisema Balozi Mapuri.**

Kuhusu ushiriki wa vyama vya kisiasa katika hatua hiyo, Balozi Mapuri alisema vitashiriki kwa kuweka wakala kila kituo cha kujiandikisha wapigakura lengo likiwa ni kushuhudia na kujiridhisha na taratibu zitakazotumika wakati wa uboreshaji wa majaribio wa daftari hilo.

Mwakilishi wa Asasi za Kiraia, Deogratius Kahumbi, aliishauri Tume hiyo kutafuta mbinu mbadala ya kuwabaini wapigakura wasiokuwa na sifa na kuwaondoa ili uchaguzi unapofika iwe rahisi kumaliza kwa wakati.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Buriani (katikati), akikabidhi vifaa vya ufugaji wa nyuki kwa Mwenyekiti wa Wajasiriamali katika Wilaya ya Uyui, Hobokela Mwansisya ikiwa ni sehemu ya Kampuni ya JTI Leaf Services kurudisha kwa jamii na kuwawezesha watu wanaoishi na ulemavu kujitegemea, mjini Tabora juzi. Wa tatu kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya JTI Leaf Services, Spika wa Bunge mstaafu, Anne Makinda na viongozi waandamizi wa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mgambo waomba udhibiti ajira wasio na mafunzo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAHITIMU wa mafunzo ya Jeshi la akiba 'Mgambo' wilayani hapa, wameiomba serikali kuweka udhibiti katika kampuni za ulinzi binafsi ili ziache kuajiri vijana wasiokuwa na sifa katika kazi za ulinzi hali inayopunguza ufanisi kwenye kazi hiyo.

Wametoa ombi hilo juzi wakati wa kufungwa kwa mafunzo ya jeshi hilo kwa vijana 56 kutoka Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama na kuomba kampuni hizo kutoa kipaumbele kwa wahitimu wa mafunzo hayo ambao wamefundishwa mbinu mbalimbali za ulinzi na usalama wa raia.

Mmoja wa wahitimu hao, Timotheo Edward, alisema wamiliki wa kampuni binafsi za ulinzi wanaogopa kuajiri vijana waliopata mafunzo ya kijeshi kwa kigezo cha gharama za mishahara na kuajiri wasiokuwa na mafunzo kwa kuwalipa fedha kidogo.

Alisema, ili kuondoa utaratibu huo ni vema serikali ikaingilia kati na kuwataka kuajiri vijana wenye sifa kama wao au kutoka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na watakaobainika kwenda kinyume wawajibishwe kisheria.

Awali, akitoa taarifa ya mafunzo hayo mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, Mkuu wa Jeshi la Akiba, Meja Nagunwa Kingu, alisema wahitimu hao wamewapatia mafunzo mbalimbali ya kukabiliana na vitendo vya kihalifu ikiwamo mbinu za kivita.

"Pia wamefunzwa usomaji wa ramani, ulengaji wa shabaha, kwata, uraia na uhamiaji ili kusaidia ulinzi wa jamii na kukabiliana na uvamizi katika maeneo mbalimbali watakapofanya kazi," alisema Meja Kingu.

Mkuu wa wilaya hiyo, Mhita, alisema watafanya uhakiki wa kampuni za ulinzi wilayani humo ili kujiridhisha kama zinatekeleza takwa la kisheria la kuajiri walinzi wenye sifa katika kazi za ulinzi.

"Hii itaenda sambamba na uhakiki wa uboreshaji wa stahiki za watumishi wao hali ambayo itaongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao na kutoingia tamaa ya wizi wakati wa kazi," alisema Mhita.

Aidha, aliwahakikishia wahitimu hao kuwa ofisi yake itawapa ushirikiano kwa kusimamia na kuratibu mafunzo kwa kushirikiana na mshauri wa mgambo ili kuhakikisha hakuna atakayeajiriwa asiyekuwa na sifa stahiki.

# Viongozi CBWSO wakanywa wizi ankara za maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VIONGOZI wa vyombo vya watoa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSO), mkoani Shinyanga wameonywa kujihusisha na wizi wa fedha za ankara za maji na watakaokaidi watafunguliwa kesi ya uhujumu uchumi.

Hayo yalibainishwa juzi na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Dafroza Ndalichako, wakati akifungua mafunzo ya siku 10 kwa viongozi hao wa CBWSO kuhusu kukusanya ankara za maji kutoka kwenye malipo ya mkononi kwenda mfumo wa kutumia namba ya malipo 'Control Namba'.

Alisema kupitia mfumo wa malipo ya namba, hatarajii kusikia viongozi hao wanapokea malipo ya Ankara kinyume na mfumo huo na kufanya ubadhirifu wa fedha za umma.

"Hakikisheni mnaingiza taarifa zote za wateja wenu kwenye mfumo wa kielektroniki ili walipe ankara za maji kwa mfumo huu mpya na siyo kupokea fedha mkononi, kiongozi atakaye kwenda kinyume na mfumo huu hatobaki salama," alisema Ndalichako.

"Hizi ni fedha za umma na ikitokea umezitumia vibaya bila kufuata utaratibu utawajibishwa na naomba niwaambie kuwa serikali ipo makini na chombo chenu kipo kwa mujibu wa sheria ya maji namba tano ya mwaka 2019," aliongeza.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Juliety Payovela, alisema mfumo huo wa malipo ya Ankara za maji kwa kutumia namba ya malipo, utasaidia kuongeza ukusanyaji wa mapato katika mauzo ya maji.

**Alisema kupitia mfumo wa malipo ya namba, hatarajii kusikia viongozi hao wanapokea malipo ya Ankara kinyume na mfumo huo na kufanya ubadhirifu wa fedha za umma.**

"Kila robo CBWSO zinaingiza Sh. milioni 500, na hapo fedha zinakuwa mikononi mwa watu na lazima upotevu wa fedha uwepo japokuwa bado hatuna takwimu sahihi, lakini kwa mfumo huu tutadhibiti mianya hiyo," alisema Mhandisi Juliety.

Mratibu wa masuala ya fedha kwa CBWSO Tanzania, Adam Mzengi, alisema malipo hayo ya ankara za maji yakikusanywa vizuri kwa mfumo huo wa namba ya malipo, mapato yataongezeka na itasaidia RUWASA kuendelea kutekeleza miradi mingi ya maji kwa wananchi na kumtua mama ndoo kichwani.

ama
ALHAMISI NOVEMBA 23, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Waziri achachamaa 'kula sahani moja' na maduka wauza dawa bila ya cheti**



**Simulizi iliyojaa sayansi tata kwenye mti mbuyu, uliosheheni historia siku ulipoanguka Dar**

Ukurasa 13

## MDAU UASISI MKATABA PARIS – AENDELEZA VIKAONI COP…

# Mapya ya Samia kunakishi mzizi wa JK na tabianchi nyumbani hadi kimataifa

## •Pia yumo penye sauti 'mama na mazingira'

**Na Mwandishi Wetu**

HADI sasa kote duniani, nadharia mazingira imeshika kasi kwa matendo, hata ngazi ya taaluma. Ina mzizi mrefu ambao ngazi ya kushamiri kwake, Tanzania inaingia katika rekodi ya mdau mkuu.

Simulizi ndefu za kutetea usalama wa mazingira, inajumuisha miaka 58 iliyopita, Marekani wanasayansi walipompa tahadhari Rais Lyndon Baines, janga la mazingira dunia iendako.

Kimsingi, ndiko ilikofika sasa nyenzo ya kupigania fimbo maalum iitwayo 'COP' inatumika kukabili ongezeko la joto duniani na athari tabianchi, sura kuu inatoka kwenye makubaliano makuu duniani yaliyofikiwa mwaka 1997 ikiunda sura ya pamoja.



Rais Samia Suluhu Hassan, akijadili mada katika mkutano ulioandaliwa na Benki ya Dunia, kuhusu miradi ya mazingira inayopunguza hewa ukaa kwenye kikao cha COP 27 nchini Misri, Novemba, mwaka jana. Mkutano uliongozwa na Rais wa Benki ya Dunia, David Malpass, pia ukahudhuriwa na Rais wa Msumbiji, Filipe Nyussi. **PICHA: MTANDAO.**

**MAZINGIRA NCHINI**

Nchini Tanzania miaka miwili kabla ya makubaliano hayo ya mwaka 1997, kukashuhudiwa muundo wa kiserikali, Wizara Mazingira inaundwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Hiyo ni katika zama Awamu ya Tatu, uongozi wa Rais Benjamin Mkapa, aliyeanza mwaka 1995, hadi 2005.

Sura nyingine husika, ni katika uongozi wa Awamu ya Nne kwa Rais Jakaya Kikwete, aliyeanza mwaka 2005, kufika mwaka 2010 akampata Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Samia Suluhu Hassan.

Hapo kwa namna ya pekee, Dk. Samia akapata ujuzi mpana kusimamia mazingira, sekta nyeti kitaifa na kimataifa, huku mkuu wake Rais Kikwete katika uongozi wake wa miaka 10, mwishoni akachaguliwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ya Umoja wa Afrika (AU).

Kamati hiyo ikawa na jukumu la kuongoza nchi za Afrika kupanga mikakati, mbinu na njia za kukabiliana na madhara ya tabianchi na kutumia changamoto zake, kuleta maendeleo kwa Afrika

Ni kamati anayoiongoza Rais Dk. Kikwete, ikawa na wajumbe wakuu wa nchi za; Algeria, Ethiopia, Congo Brazaville, Kenya, Mauritania, Mauritius, Msumbiji na Uganda.

Katika ajenda zake, ikawa inasisitiza nchi za Kiafrika, kuboresha uwezo wa kupata taarifa za tahadhari zote, fedha, mawasiliano na usafirishaji katika miji yake, zikizuia mafuriko kwa njia za kisasa, kupanga miji na kupunguza athari.

Ndii kipindi harakati za Umoja wa Mataifa (UN) kuelekea Mkataba wa Paris wa Mazingira, zikawa zimepamba moto, nchini kukiwapo ubia wa kiutendaji kati ya Rais Kikwete mwenye dhamana kimataifa na waziri wake wake, Dk. Samia, anayesimamia mazingira.

Pia, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Ban Kin Moon, akaanzisha mawasiliano na Kikwete kueneza ushawishi wake kwa ajenda ya dunia, Mkataba wa Paris kupitia kivuli cha AU kwa Afrika, mtekelezaji kiserikali nyumbani akiwa Samia.

Mnamo Juni 2014, kwenye kikao cha AU jijini Malabo, Guinea ya Equator, Ban Kin Moon akatembelea Kamati ya Mazingira chini ya Kikwete, akateta nayo kuhusu kudai ushirukiano wa ajenda ya Paris ya 2015, ambayo mwanzo wake ukawa kikoa cha Septemba, 2014 nchini Marekani, Rais mstaafu Kikwete akingia katika timu ya Katibu Mkuu UN kufanikisja mkakati.

**JK ALIPOSTAAFU**

Hiyo ikajenga mzizi wa kina nchini baada ya uchaguzi wa mwaka 2015, zama Awamu ya Sita, Dk. Samia akawa amepanda daraja, yu msimamizi na mhudumiaji moja kwa moja wa mazingira kitaifa, katika nafasi yake Makamu wa Rais.

Wakati Mkataba wa Paris ulishafikiwa miezi kadhaa kabla ya Rais Kikwete kustaafu, zama za Awamu ya Tano chini ya rais JohN Magufuli, Samia akawa amebaki ni kada mwenye ujuzi na hisitoria hai ya Tanzania na Mazingira, akiwa msimamizi mkuu kitaifa.

Inaendelea Uk. 12

AFYA

# Waziri achachamaa ‘kula sahani moja’ na maduka wauza dawa bila ya cheti

## • Adai ya antibaiotiki yanampandisha hasira

**Na Yasmine Protace**

HIVI sasa kuna maduka mengi ya dawa, mjini na vijijini kuwahudumia wahitaji kwa vigezo na masharti.

Inawezekana mgonjwa akaenda kituo cha afya, hospitali au zahanati, wakapata vipimo na kuandikiwa dawa, lakini dawa zinaweza zisiwapo na akapewa kibali aende kununua dawa katika maduka yanayouza dawa hizo.

Hilo ni jambo jema kitaifa na kisera, mtu anapata dawa kupitia utaratibu wa daktari kwa kuandikiwa kibali tena kilicho na idhini.

Ndani ya utaratibu huo, kunatajwa kuwapo mazoea kwa baadhi ya watu wanasumbuliwa na maradhi, badala ya kwenda hospitali, hawafuati utaratibu sahihi wanaenda kunakouzwa dawa, na wanazipata bila ya kuwa na kibali.

Ni hali inatajwa kuchangia watu kupata usugu wa dawa, kutokana na kutofuata utaratibu walioweke-wa.

Sasa kisheria na kisera, inatajwa ni jukumu la mafamasia, pia mmiliki wa duka husika la dawa, kuhakikisha waliowaajiri, hawatoi dawa bila ya kukabidhiwa kibali kutoka kwa wataalamu sahihi wa afya.

Hivi karibuni Waziri wa Afya Ummy Mwalimu amesema kuwa wafamasi na wamiliki wa maduka ya dawa, wanatakiwa kutoa dawa kwa kuangalia cheti cha daktari na si kinyume cha hapo.

Waziri Ummy anasema, kama dawa zitaendelea kutolewa bila ya kupokea cheti, hali hiyo itachangia kuwapo kwa tatizo la usugu na vimelea. vya magonjwa dhidi ya dawa na kuhatarisha afya za watu.

Anatamka hilo katika tukio la kufunga Kongamano la Tatu la Usugu wa Vimelea dhidi ya Dawa na kufungua rasmi wiki ya uhamasishaji na uelimishaji jamii, matumizi sahihi ya dawa darasa la wiki moja linalohitimishwa kesho.

Kongamano hilo linaolofanyika jijini Arusha, waziri anatoa agizo lenye ufafanuzi, kwamba:

“Nataka wafamasia wote nchini, kuacha mara moja tabia ya kutoa dawa ikiwamo za antibiotiki bila ya cheti cha daktari na nikimkamata mtu siku moja, nitampiga faini kubwa, kama sio kumfungia duka kabisa.”



Shughuli zikiendelea ndani ya duka la dawa, Waziri Ummy Mwalimu, akisisitiza vigezo na masharti ni muhimu katika utendaji wa maeneo hayo. **PICHA: MTANDAO.**

Hapo anaahidi kutumia timu mahsusi kufanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka ya dawa, akisisitiza kuwa mfamasia atakayebainika kutoa dawa, hasa za antibaiotiki bila ya cheti cha daktari, atafikishwa mahakamani ambako kuna sheria inayotoza faini kubwa.

Aidha, Waziri Ummy anawataka wataalamu wa afya kuzingatia Mwongozo wa Taifa wa Matibabu, wanapowahudumia wagonjwa, ili kufanikisha kampeni ya ‘Afya Moja’ yenye lengo la mapambano ya usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa.

“Naendelea kusisitiza kwa wataalam wetu wa Afya, hakikisheni mnazingatia ‘Mwongozo wa Taifa wa Matibabu’ Nawaomba sana hasa katika kuwaandikia wagonjwa dawa, maana tumepata kesi tunaona mtu ana UTI anaandikiwa antibiotic mpaka saba,” anatamka waziri.

Anasema iwapo watoa huduma za afya watafuata Mwongozo wa Taifa wa Matibabu, itaiwezesha serikali kwenda kwa kasi katika mapambano ya usugu wa vimelea dhidi ya dawa.

Jamal Juma, mkazi wa jijini Mwanza, anatoa uzoefu wa baadhi ya maduka ya dawa, mtu anaenda na kuongea na mtoa huduma katika duka hilo na anapatiwa huduma ya dawa.

Anasema, usahihi unatakiwa kwa watoa huduma za dawa wazingatie maudhui ya vyeti vya madaktari, ili kuondoa vimelea vya usugu katika miili ya binadamu.

Amina Jabir, anaomba elimu iendelee kutolewa kwa jamii, kwa baadhi ya watu wanapata matatizo ya kiafya, anakimbilia katika duka la dawa na kupatiwa dawa.

“ Kuna baadhi ya watu wanapojisikia vibaya kiafya, hukimbilia katika maduka ya dawa na kupatiwa dawa,” anasema.

Anaongeza kuwa, vimelea vya usugu vinaweza kupotea kama jamii iishio mijini na vijijini itakuwa na elimu ya kutosha, itakayowasaidia kuacha kukimbilia katika maduka ya dawa bila ya kuwa na cheti cha daktari.

# MAPYA YA SAMIA KUNAKISHI MZIZI WA JK NA TABIANCHI NYUMBANI HADI KIMATAIFA

**Inatoka Uk. 11**

Zao la Mkataba wa Paris wa 2015 uliotiwa saini mwanzo na nchi 196, ukazaa mkakati duniani unaopitia vikao vya nchi kila mwaka, mara nyingi vikichukua wiki mbili (COP - Conference of Parties), ajenda ni kukabili joto na mabadiliko tabianchi, ikiangaliwa kwa pekee hali ya hewa viwandani.

**SAMIA KATIKA COP**

Miezi tisa baada ya kuwa Rais Novemba mwaka 2021, Dk. Samia akahudhuria na kuhutubia kikao cha COP26, huko Glasgow Scotland, ambako akaeleza kile Tanzania na nchi nyingine zinazoendelea zinahitaji zitekelezwe.

Kauli yake ni baada ya kuhutubia mjadala wa wazi mkutanoni, kukiwapo malalamiko kwa nchi tajiri zinasuasua kutekeleza ahadi katika maguezi ya mazingira kimataifa.

Dk. Samia akanena “kwenye mkutano huu (COP26, Novemba 2021) mengi yamezungumzwa, lakini tunayopenda kusikia na tunayosukuma yazungumzwe ni sasa tutoke kwenye maneno na ahadi, twende kwenye kufanya kweli.

“Kwa sababu kila tunapokaa haya mabadiliko ya tabianchi yanaleta madhara mengi. Tunavyoendelea kubishana tutoe fedha au tusitoe, madhara yanaendelea.”

Akaendelea: “Nchi nyingi tumekubaliana, nchi zilizoendelea ziache kuvuta ahadi zao na badala yake zitoe hizo fedha haraka, ili nchi zinazoendelea ziendelee kutekeleza mipango tuliyojipangia ya marekebisho ya tabianchi.”

**MAMA NA MAZINGIRA**

Vilevile katika hatua hiyo kupokea kijiti cha mazingira kimataifa cha Dk. Kikwete, akashiriki mkutano maalum wa wanawake viongozi ulioitishwa na kiongozi wa Scotland, Nicola Sturgeon, ukimulika nafasi yao kukabili mabadiliko ya tabianchi.

Dk, Samia akawa na hoja: “Sisi wanawake viongozi wanawake tutaendelea kupaza sauti kwa ajili ya wanawake wenzetu. Tutaendelea kuwataka viongozi wa dunia kuchukua hatua zaidi kutatua changamoto zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi,

“Tunataka kuona ahadi thabiti za kupunguza kiwango cha joto hadi nyuzi joto 1.5. Tusipofanya hivyo madhara ni makubwa zaidi kwa wanawake na watoto wa kike.”

Rais Samia anaelezea jinsi Tanzania ina mkakati maalum wa kitaifa kijinsia na mabadiliko ya tabianchi wa mwaka 2013, ambao lengo lake ni kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu kukabili mabadiliko ya tabianchi.

MAZINGIRA

# Simulizi iliyojaa sayansi tata, mbuyu uliosheheni historia ulipoanguka Dar

## •Bodaboda na yao; wakongwe na enzi hizo...

**Na Mwandishi Wetu**

MTI wa Mbuyu unaweza kupewa sifa ya 'mti wa uzima' kumaanisha unaishi na kustawi muda mrefu sana, ukiwa na wasifu wa kisayansi, pia 'sayansi pori' ikiipa sifa zake za kimaabara.

Azimio la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Kuenea kwa Jangwa, unasema mbuyu unaweza kuishi hadi miaka 3,000, kukua upana hadi mita 50, na mita 30 za urefu.

Kunatajwa kuwapo aina tisa za mbuyu, sita kati ya hizo hupatikana katika kisiwa cha Madagaska, Mbuyu bado umeendelea kuwa mti usioleweka kutokana na usiri wake.

Miongoni mwa vivutio vya dunia, ni mbuyu wenye asili ya Sagole, unaopatikana nchini Afrika Kusini, ambao kutokana na upekee wake, sasa una Rekodi ya Dunia ya Guinness.

Nchini katika Makumbusho mojawapo, kunatajwa kuwapo mbuyu wenye miaka zaidi ya 50

**KILICHOJIRI TABATA**

Kuna tukio, ilikuwa majira ya saa 7.00 mchana, jua kali linawaka siku ya Jumapili hivi karibuni, kukashikika kishindo kikubwa kutikisha katika maeneo mengi ya Segerea, Dar es Salaam, jirani na mti mkubwa aina ya mbuyu, hata ukazua taharuki ya watu kukumbwa na tetemeko la ardhi.

Umma huo ukatoka kwenye majumba yao, huku wengine wakikimbia huku na kule kunusuru maisha yao.

"Nikiwa ndani ya nyumba yangu nilisikia kama tetemeko la ardhi linatikisa na baadhi ya vitu vilianguka chini, nikaogopa sana, nikajiuliza ni nini hiki tena," anasema mkazi, Kelvina Mwamba.

Mama huyo wa watoto wawili, anasema ni tukio la Jumapili, wakati wakiwa katika maandalizi ya kupika chakula cha mchana kwa familia.

Anasimulia kusikia kishindo kikubwa na alipotoka nje hakujua kilichotokea, ila baadaye akawaona majirani zake wakikimbia kutoka kwenye nyumba zao.

Kelvina anaeleza kadri muda ulivyoenda, watu walitoka kwenye makazi yao na kukusanyika katika makundi, wakihoji na kuijadili kishindo hicho, wakichukua tahadhari ya kilichojiri.

Hapo Kelvina anasimulia, ghafla wakatokea vijana waendesha bodaboda wakishangilia, huku wakipiga honi kuzunguka maeneo ya makazi yao.



Viongozi wa Mtaa wa Machicha, Tabata , Dar es Salaam, wakikagua mti wa mbuyu ulioanguka na kuziba barabara. **PICHA: JOHN BADI.**

"Tulipigwa butwaa kwa kitendo cha hawa bodaboda, kila mmoja wetu akawa anajiuliza sababu za wao kuzunguka wakipiga honi, yowe huku wakinyanyua mikono juu," anasema.

Jirani mwingine, Michael George, anasema njiani wakati anarejea akaisikia watu wakisema 'mbuyu umeanguka.'

George anasema, baada ya kupata taarifa hizo, akaenda moja kwa moja kwenye eneo la tukio kushuhudia ukweli wa mbuyu huo ulivyoanguka, hata ukafunga barabara inayounganisha maeneo ya Tabata Chang'ombe kwenda Tabata Kisukulu, Dar es Salaam.

Mashuhuda wanaeleza ni tukio mbalo halikuwa na madhara kwa wapita njia, pia wakazi jirani. Anaendelea; "Mahali ulipo mbuyu pamoja na kuwa kijiwe cha bodaboda, ni makutano ya barabara ya kutoka Kimanga kuelekea Machimbo, Chang'ombe hadi Majichumvi Kisukulu."

"Kwangu mimi naona maajabu, kwa sababu wakati ukianguka hakukuwa na bodaboda aliyekuwapo, haukusababisha maafa kwa maana ya vifo, uharibifu wa mali kama kubomoa nyumba na kuharibu magari."

Mzee Hamisi Kambaulaya, anasema mbuyu huo una miaka mingi na kuanguka kwake, huenda umetokana na kuzeeka, binafsi akiufahamu tangu akiwa na wazazi wake mahali hapo, alipoishi muda mrefu.

"Watu wengi walikuwa wanaishi katika maeneo hayo kwa ajili ya kukata miti kwa ajili ya kupasua kuni na kuchoma mkaa," akidokeza ni eneo lililotawaliwa na pori na wao waliishi kwa kuhamahama, wakiwa na makazi ya nyasi.

Mkazi mwingine, Emmanuel Thobias (55), anasema wakati wazazi wake wanahamia katika eneo hilo la Machimbo, kulikuwapo pori lenye miti mingi mikubwa, ukiwamo mbuyu huo na wanyama kama simba, nyoka na ndege aina ya bundi na nyumba ndogo za kufanyia matambiko ya ukoo.

Anasema katika maeneo hayo, majira ya saa 1.00 usiku walikuwapo wakiwaona watu wakiwa wamevaa mavazi meupe, kichwani wamefunga vilemba, wameongozana wakielekea kwenye vibanda hivyo.

"Ilikuwa ni kawaida wazazi wetu kukutana na watu hao, walikuwa hawazungumzi na mtu yoyote wala kugeuka wanapokutana nao," anatamka.,

Anarejea kuwapo madai, watu hao walikutana kwenye mbuyu huyo kwa ajili ya kufanya matambiko.

"Ili eneo lote lilikuwa na vibanda vingi vya matambiko, mwanzoni tulikuwa tunaogopa, lakini baadaye tuliizoea hiyo hali, tukawa tunaona ni mambo ya kawaida tu," anasema.

**YA BODABODA**

Bodaboda, Henry Komba anataja hisia zake, kwamba mbuyu huo unatumika kwa mambo ya kishirikina, kwa sababu baada ya kuanguka, ndani yake kulikuwapo shimo kubwa lenye vyungu, majiko, sahani, bakuli, vijiko na vikombe.

Pia, kukawapo vyakula; mchele, mahindi, karanga, uwele, ufuta na ulezi. Henri anaendelea: "Kuna wakati mwingine ukiwa unasubiri abiria, unasikia watu wanaongea, lakini huwaoni. Hali hiyo ilikuwa inatutisha sana, kiasi kwamba mtu hawezi kukaa pekee yako kwenye kijiweni."

Mwendesha bodaboda mwingine aliyejitambulisha kwa jina Shoshosho, ana madai:"Unawaona watu wamesimama au wamekaa wanaongea, ukigeuka kidogo tu, ghafla unakuta wametoweka... dunia hii jamani kuna mambo!"

**WENYEJI MTAANI**

Boniface Ngimwa, anayeishi jirani na mbuyu, anadai nyakati za usiku wamekuwa wakishuhudia vihoja vya sauti za watu na wanapotoka nje, hawawaoni.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Machimbo, Mariamu Machicha, anathibitisha kuanguka mbuyu, ila anapinga madai ya ushirikina, kuwa na matamshi: "Unajua watu wanaweza kudhani hivyo kwa sababu mti huo ulikuwa uko njia panda ambako kuna makutano ya Barabara."

Machicha anaiaomba Nipashe kuwa,wakati mti huo unaanguka hakukuwapo bodaboda na uliangukia kwenye barabara inayotoka Tabata Chang'ombe hadi Majichumvi, ikaziba njia.

Anaeleza jitihada zilifanyika kuukata mti huo, kwa ushikirikiano na wakazi wa eneo hilo, aliyetoa vifaa na hakukuwapo madhara.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Machimbo, Mariamu Machicha anasema baada ya kupata taarifa za kuanguka mbuyu, Kamati ya Ulinzi na Usalama, ilienda kwenye eneo la tukio kuimarisha ulinzi na ndiko wasamaria jirani wakauwaunga mkono, hata kuwezesha Barabara kufunguka.

Nipashe ilipotaka kujua ukweli wa kukutwa vifaa vya mapishi mahali, akajibu: "Nadhani ni imani tu, kwa sababu mti huo ulikuwa kwenye makutano ya barabara, mtu anaweza kudhani hivyo tu."

**MBUYU NI NINI?**

Ni mti unaopewa sifa 'mti wa uzima' kumaanisha unaoishi na kustawi muda mrefu sana na kutanuka na kuenea zaidi, ikizungukwa na kila aina ya itikadi na maajabu ya kisayansi.

Azimio la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Kuenea kwa Jangwa, mti wa mbuyu unautaja unaweza kuishi hadi miaka 3,000, kukua upana wa hadi mita 50, na kufikia hadi mita 30 kwa urefu.

Kuna takribani aina tisa za mbuyu, sita kati ya hizo hupatikana katika kisiwa cha Madagaska na mti wa mbuyu wenye asili ya kuvutia ujulikanao kama Sagole, unaopatikana nchini Afrika Kusini, ambao kutokana na upekee wake hadi sasa unamiliki rekodi ya dunia ya Guinness.

Mbuyu pia kitaalam hufahamika kama mti ulioota juu chini, kwa sababu unaonekana kana kwamba mizizi yake inamea juu angani.

Lingine, lisilojulikana sana, majimaji yake yana tindikali ianyotosha kutumika kugandisha maziwa, kupikia, kuoka na kutengeneza kileo.

MAZINGIRA

# Mafuriko yanavyochochea ufukara Afrika

## •Vifo, vilio makazi, mifugo na miundombinu

Na Maulid Mmbaga

HIVI sasa janga la mafuriko kimataifa ni tatizo kubwa duniani, hasa barani Afrika, ikibainishwa changamoto inayosababisha maafa zaidi katika vipindi vya mvua, kutokana na miundombinu duni inayozunguka makazi ya watu.

Tanzania imo katika orodha barani Afrika ya nchi zinazokabiliwa na mafuriko mara kadhaa na kushuhudiwa maafa, katika mikoa kama Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Morogoro, Mbeya, Pwani na Mara.

Ni mfano hai wakazi wa Dar es Salaam wanakumbwa na mafuriko hayo, kila inapofikia majira ya mvua na baadhi wakipoteza mali zao, amani, makazi na mifugo, huku miundombinu kama barabara na madaraja zikiharibika.

Athari zake sasa, hata shughuli za kijamii zinasimama kutokana na mafuriko, hilo linathibitika mkoani Dar es Salaam, baada ya mamlaka ya jiji kufunga baadhi ya Barabara, kama vile Morogoro inayopita eneo la Jangwani na Kigogo.

Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA), ilitoa tahadhari kuhusiana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha na kuagizia uwezekano wa kutokea uharibifu wa miundombinu na makazi ya watu, ambayo tayari umeshashuhudiwa kutokea.



Wananchi wakiangalia makazi yao yaliyojaa maji, baada ya mafuriko katika eneo la Kigogo, Dar es Salaam. **PICHA MAULID MBAGA.**

### KAULI YA SERIKALI

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, anasema serikali ina mipango ya muda mrefu kujenga daraja eneo la Jangwani, kunakokumbwa na mafuriko ya kila mara, hata kufanyiwa marekebisho ya muda mfupi, ikiwamo kuondoa tope na kusafisha mifereji.

Pia, anawaelekeza wakuu wa mikoa na wilaya nchini, kutoa elimu kwa wananchi kuzingatia usafi, kutokutupa taka ovyo, jambo analolitaja kuchangia mifereji na madaraji kuziba, hata kusababisha maji kushindwa kupita vizuri kwenye njia zake.

"Niipongeze mamlaka ya hali ya hewa, ilitoa tahadhari mapema, lakini mabadiliko ya tabianchi hakuna anayejua kesho yatakuja kwa njia zipi.

"Tunawaahidi Watanzania, tutaendelea kujipanga kama serikali kujua tunakabiliana vipi na mafuriko," anasema Bashungwa.

Mkurugenzi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Meja Jenerali Charles Mbuge, anaeleza serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano na sekta katika kukabiliana na maafa, kuhakikisha umma unaishi kwenye mazingira salama.

### HALI YA UGENINI

Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), nalo linasema mamilioni ya watu wanaathiriwa na mafuriko Afrika Magharibi na Kati, eneo lililogubikwa na migogoro, pia umaskini.

UNHCR inataja mafuriko makubwa na mabaya zaidi katika muongo mmoja uliopita, hata kusababisha watu zaidi ya milioni 3.4 kukoseshwa makazi nchi za Nigeria, Chad, Niger, Burkina Faso, Mali na Cameroon.

Shirika hilo linasema, Kaskazini Mashariki mwa Nigeria, mafuriko yameathiri watu milioni tatu, ikaua mamia na kuwakosesha makazi zaidi ya watu milioni 1.3 amboa pia wameharibiwa makazi yaliyokuwa yakihifadhi zaidi ya watu milioni mbili.

Msemaji wa UNHCR, Olga Sarrado, anasema Chad ilitangaza dharura baada ya mafuriko yanayowaathiri zaidi ya watu milioni moja, mito ikafurika hadi kwenye kingo zake, mashamba kufunikwa, mifugo kufa na kuwalazimisha watu 90,000 kukimbia nyumba zao.

"Katika nchi za Sahel ya Kati, Burkina Faso, Niger, na Mali mvua kuliko viwango vya wastani na mafuriko yameua mamia ya watu, maelfu kukoseshwa makazi na takriban hekta milioni moja zimeharibiwa.

"Hali mbaya sana ya hewa katika eneo la Sahel, imechochea ukame na mafuriko, kushusha viwango vya mazao na kuchangia kwa jumla kudorora huduma za umma na kusababisha ukosefu wa makazi," anatamka Sarrado.

### SUDAN KUSINI

Nchini Sudan Kusini, nako ni miongoni mwa mataifa yanayotajwa kukabiliwa na mafuriko kwa kipindi kirefu, mwaka 2021 mvua kubwa zilinyesha na kuathiri barabara, madaraja na viwanja vya ndege, huku zaidi ya wakazi 700,000 wa jimbo la Jonglei, wakibaki bila msaada, sehemu kubwa ya eneo lao liokijaa maji.

Pia inabainishwa athari zilizoletwa na mafuriko, zikijumuisha nyumba kusombwa na maji, mashamba kuharibiwa, huku wenye mifugo wakilazimika kuihamishia maeneo ya juu katika miji jirani, wakazi wakihangaika bila ya chakula, maji na huduma za usafi wa mazingira.

Inaelezwa, mnamo Agosti 2022, Sudan Kusini ilikumbwa na mafuriko, watu 52 walifariki na nyumba 8,000 zikaharibiwa.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuratibu Masuala ya Kibinadamu na Misaada ya Dharura (OCHA), linaonyesha wasiwasi kwa maisha ya Wasudan yanatishiwa, huku vyanzo vya maji kama visima vikizamishwa katika maeneo mengi nchini humo.

Hata hivyo, UNHCR inashauri mabadiliko ya tabianchi yasiwe chanzo cha watu kukata tamaa kwakuwa suluhisho la mafuriko ni pamoja na kutenganesha mifereji na mipango mizuri ya miji.

### DRC NA MSUMBIJI

Mwaka 2022, inaelezwa zaidi ya watu 120 walipoteza maisha kutokana na mafuriko kwenye mitaa 24, ilioyokuwa inakaliwa na zaidi ya watu milioni 12 katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), huku ikisadikika vifo vingi hasa vya watoto, baada ya nyumba zao kuanguka.

Pia mwaka huu, inabainishwa zaidi ya watu 500 wamefariki kutokana na mafuriko, pia maporomoko ya matope katika wilaya ya Kivu.

Vilevile, Shirika la Afya Duniani (WHO), linaonya kuwa mafuriko yanayotokana na mvua Kusini mwa Afrika, yanaongeza hatari ya ugonjwa kipindupindu.

Kwa mujibu wa WHO, timu za kukabiliana na ugonjwa huo zinapata changamoto ya kuwafikia wanaohitaji huduma, kutokana na miundombinu mibovu iliyoharibiwa na mafuriko.

Vilevile inatathminiwa na WHO, kwamba mafuriko yameathiri zaidi ya watu 44,000, vituo vya afya 55 na inakadiriwa kilomita 3,500 za barabara zimeharibika na kumeshuhudiwa ongezeko kubwa la athari tangu Desemba 2022 wakati wa msimu wa mvua.

### BARANI ULAYA

Kwa mataifa ya Ulaya ya Kati, yanatajwa kukabiliwa na dharura ya mvua kubwa inayoendelea kunyesha na kusababisha mafuriko yaliyovunja rekodi, pia kuwapo maporomoko ya udongo.

Inakadiriwa, mataifa yaliyoathirika zaidi ni Slovenia, Austria na Croatia ambazo ni za nchi jirani, nako kuna vifo vya watu sita vimeripotiwa.

Waziri Mkuu wa Slovenia Robert Golob, anakadiria hasara iliyotokana na mafuriko hayo, imefikia Euro milioni 500 (sawa na shilingi bilioni 1.368 (Sh.

1,367,623,775,0000), jambo linalomfanya kuomba msaada wa haraka kutoka Umoja wa Ulaya (EU) na Jumuiya ya Kujihami ya NATO.

Inaelezwa, kingo za mito mikubwa mitatu nchini humo zimepasuka na baadhi ya vijiji, barabara na njia za reli zimefunikwa na maji.



Barabara iliyoharibika vibaya kutokana na mafuriko nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). **PICHA ZOTE MTANDAO.**



## Serikali, wadau waona fursa mifumo ya chakula

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya kilimo ili kuleta mabadiliko katika sekta hiyo na kutumia fursa zilizopo kwenye mifumo ya chakula.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao wa Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimago alitoa kauli hiyo jana alipofungua Jukwaa la Wadau wa Kilimo Wasio wa Kiserikali (ANSAF) kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo.

Alisema eneo kubwa ambalo serikali inasisitiza ni matumizi ya teknolojia ili kuboresha mifumo ya chakula nchini.

"Ni lazima tuongeze tija kwenye kilimo, tunahitaji kupiga hatua mbele kama Rais alivyoamua kuwekeza katika kilimo," alisema Chimagu.

Alisema malengo waliojiwekea katika Mkutano wa Kimataifa wa Mifumo ya Chakula (AGRF) ni sekta binafsi kuwekeza na kutumia fursa zilizopo kwenye sekta ya kilimo.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo, Dk. Daniel Mushi, alisema sekta binafsi zinatakiwa kutumia fursa za mkutano wa AGRF ili kupaisha sekta ya kilimo na mifugo.

Alisema itakuwa ajabu kwa Watanzania kushindwa kutumia fursa hizo wakati mkutano huo ulifanyika nchini na nchi mbalimbali zilihudhuria na kutangaza fursa.

Alisema Tanzania haina sababu ya kuagiza mazao nje kwa sababu ardhi wanayo na wataalamu wa kilimo wapo.

Mkurugenzi Mtendaji wa ANSAF, Honest Mseri, alisema kuna haja kuongeza uzalishaji kwenye kilimo ili kukidhi mahitaji yaliyopo na kuimarisha mifumo ya chakula.

# Wachambuzi wa mifumo ya TEHAMA wapewa angalizo ubunifu akili bandia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAIMU Meneja wa Ushauri na Uelekezi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), amewataka wachumbuzi wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye taasisi za umma kuongeza elimu na kupata maarifa mapya ili kuendana na kasi ya ukuaji wa mabadiliko ya teknolojia mpya zinazoibuka ikiwamo akili bandia.

Joan Valentine alitoa maagizo hayo jana alipofungua mafunzo kwa wachambuzi hao jijini hapa, akisema kuwa kutokana na kasi ya ukuaji wa teknolojia, wachambuzi wanapaswa kuendana na wakati kwa kujifunza stadi mbalimbali za teknolojia ya akili bandia na uchambuzi wa takwimu, ili ziwasaidie kupambana na mabadiliko ya teknolojia.

"Kwa sasa dunia inazungumza kuhusu akili bandia, hivyo wachambuzi wa mifumo lazima muwe na ujuzi wa hizi teknolojia ili kuzisaidia taasisi zenu katika utendaji kazi wa kila siku.

"Ni muhimu kujifunza stadi tepe (soft skills) ili ziweze kuwasaidia katika kupambana na mabadiliko yanayoendelea kutokea katika TEHAMA ulimwengu kote," alisema.

Mratibu wa Mafunzo hayo, Ceaser Mwambani ambaye ni Mchambuzi wa Mifumo ya TEHAMA kutoka e-GA, alisema lengo la mafunzo hayo ni kujengea uwezo maofisa hao katika maeneo ya uchambuzi wa mifumo ya TEHAMA, usimamizi wa miradi ya TEHAMA, miongozo, viwango, usimamizi, ubora na usalama wa mifumo ya TEHAMA serikalini.

"Kupitia mafunzo hayo tuna imani kuwa washiriki wote hapa watakuwa na uelewa zaidi kuhusu uchambuzi wa mifumo na miradi ya TEHAMA pamoja na kutoa mchango mzuri kwenye taasisi zao ili kuwa na miradi yenye tija kwa taifa," alifafanua.

Mafunzo hayo yanayotarajiwa kukamilika kesho, ikiwa ni mwendelezo wa jitihada za e-GA kuhakikisha inashirikiana na kuzijengea uwezo taasisi za umma katika kukuza serikali mtandao.



Mkurungenzi Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Justina Mashiba akizungumza na wajumbe wa Kamati ya mawasiliano, ardhi na nishati wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, walipotembelea ofisi za mfuko huo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wanafunzi msingi, sekondari wapewa elimu kuhusu sheria

**Na Thobias Mwanakatwe**

TUME ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT) imeanza kutoa elimu kuhusu sheria mbalimbali katika shule za msingi na sekondari za Mkoa wa Rukwa ili kuongeza uelewa na utii wa sheria bila shuruti.

Mkuu wa Kitengo cha Elimu ya Sheria kwa Umma, Zainabu Chanzi, katika taarifa aliyotoa kwa vyombo vya habari jana, alisema kuwa moja ya majukumu ya tume hiyo ni kutoa elimu kwa umma ili kuisaidia jamii kuzielewa sheria na hivyo kupunguza utendaji makosa mbalimbali ya jinai.

Chanzi alisema elimu hiyo kwa shule hizo ni pamoja na Sheria ya Mtoto, makosa dhidi ya maadili ya utu, makosa ya kimtandao, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Katibu Tawala Mkoa wa Rukwa, Gerald Kusaya, aliipongeza tume kwa kutoa elimu hiyo kwa wanafunzi. Itakuwa na tija kubwa kwa jamii na kusaidia watoto kufahamu haki na wajibu wao na kujiepusha kutenda makosa mbalimbali yaliyoanishwa katika sheria husika.

Katibu Tawala huyo aliiomba tume hiyo kuendelea kutoa elimu hiyo kwenye shule na vikundi mbalimbali vya vijana na wajasiriamali kwa kuwa uelewa wa sheria utasaidia wananchi kutii sheria bila shuruti.

Kusaya alishauri elimu hiyo kuendelea kutolewa katika makundi mbalimbali ya jamii bila kusubiri watende makosa kufikishwa mahakamani.

## Soko kufanyiwa maboresho

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema Soko la Majengo jijini Dodoma litafanyiwa maboresho ili liwe na hadhi ya makao makuu ya nchi kutokana na baadhi ya miundombinu yake kuchakaa.

Akizungumza na wafanyabiashara wa soko hilo jana, Senyamule alisema, "soko linakuja kujengwa kwa viwango vya majengo ya Jiji la Dodoma, kwa hadhi ya makao makuu ya kisasa.

"Lazima huduma za soko hili ziendane na sura ya makao makuu ya nchi. Maboresho ni lazima yafanyike kwa utaratibu uliowekwa na serikali wa kukaa, kushauriana na kukubaliana kwani yamo kwenye sera ya nchi ya maboresho ya masoko," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema soko hilo lina wafanyabiashara 220, kila mmoja anahudumia wateja kuanzia wanne hadi watano kwa siku, hivyo takribani watu 10,000 kwa siku wanahudumiwa huko.

Alisema kuwa kwa kuzingatia umuhimu huo wa utoaji huduma kwa wananchi, maboresho ni lazima kufanyika kwenye soko ili kuwa na mazingira rafiki kwa wateja.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji, Francis Kaunda, alisema vyanzo vya mapato ya soko hilo vinakusanywa moja kwa moja na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kutoka kwa wafanyabiashara na vingine vinakusanywa na wazabuni.

"Kuna kodi ya pango kwa ajili ya vibanda na meza, ushuru wa vyoo, mizigo inayoingia sokoni pamoja na ada za mikataba na makisio ya mapato kwa mwaka ni Sh. milioni 204.7.

"Halmashauri ya Jiji la Dodoma hukusanya ada ya leseni pamoja na ushuru wa huduma kutoka kwa wafanyabiashara waliopo ndani ya soko wenye sifa za kupewa leseni," alisema.





# Kampuni yatoa mil. 48/- huduma za kijamii

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

KAMPUNI ya Ununuzi wa Tumbaku ya Premium Active Tanzania, imekabidhi hundi ya Sh. milioni 47.8 kwa kata tisa za wilaya za Chunya mkoani Mbeya na Songwe kama sehemu ya uchangiaji wa huduma za jamii (CSR).

Mfano wa hundi ya fedha hizo ilikabidhiwa juzi na Meneja Shughuli wa Kampuni hiyo, Nico Royssos, kwenye hafla maalum iliyofanyika kwenye ofisi za kampuni, Lupa Tingatinga wilayani hapa.

Roysss alisema fedha hizo zimetolewa na kampuni hiyo kwa ajili ya kuchangia huduma za kijamii hasa katika sekta za elimu na afya kwenye kata tisa ambazo ndizo zinajihusisha na kilimo cha tumbaku katika wilaya hizo mbili.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 9.34 ni kwa ajili ya kata tatu za wilaya ya Songwe na Sh. milioni 38.4 kwa ajili ya kata sita za wilaya ya Chunya ambayo ndiyo yenye eneo kubwa la uzalishaji.

"Utaratibu wa kutoa fedha hizi unazingatia kiwango cha uzalishaji katika kila kata ndiyo maana kwenye huu mgawo, Chunya inapata fedha nyingi zaidi kuliko Songwe japokuwa sisi hili eneo lote ni mkoa wa kitumbaku," alisema Royssos.

Alizitaja kata zinazonufaika na fedha hizo kuwa ni Lualaje, Kambikatoto, Matwiga, Mtanila, Lupa tingatinga na Nkung'ungu za wilayani Chunya na Kapalala, Ngwala na Gua za wilaya ya Songwe.

Ofisa Uhusiano na Usimamizi wa Premium Active Tanzania, Yusuph Mahundi, alisema katika msimu uliopita wa ununuzi wa tumbaku kwa wilaya ya Chunya, walinunua kilo milioni 6.4 zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 16.

Kwa wilaya ya Songwe, kampuni hiyo ilinunua kilo milioni 1.5 zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 3.7. mbali na mchango huo wa kwenye huduma za kijamii pia wamelipa malipo mbalimbali kwenye halmashauri.

"Kwa msimu ujao wa kilimo tumeingia mkataba na vyama saba vya msingi na kwa wilaya ya Songwe tumeongeza vyama vingine tisa. Kwahiyo endapo hili zao litakuwa endelevu tutafanya mambo mengi makubwa," alisema Mahundi.

Akizungumza kwa niaba ya madiwani wa kata zinazozalisha tumbaku, Diwani wa Mtanila, Nickson Mwakuga, aliiomba kampuni hiyo kuendelea na utaratibu huo wa kuchangia huduma za kijamii kwa wananchi.


Alisema, kampuni hiyo imekuwepo wilayani humo kwa muda mrefu na imekuwa ikitoa ushirikiano kwa wananchi hasa wakulima wa zao hilo ambalo ni miongoni mwa mazao ya kimkakati kwa sasa.

Akipokea hundi hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Simon Mayeka, aliishukuru kampuni hiyo kwa kuiunga mkono serikali kwenye uboreshaji wa huduma za kijamii katika wilaya yake.

Mayeka aliwataka madiwani na viongozi wengine wa serikali kwenye maeneo yanayonufaika kuhakikisha wanasimamia fedha hizo ili zilete matokeo Chanya na kwamba atafuatilia ili kuhakikisha zinaleta matokeo yanayokusudiwa.

"Hizi fedha si za kulipana posho kwahiyo hatutarajii kusikia watu walikuwa wanalipana posho. Fuatilieni na mtusaidie kusimamia, fedha hizi zilizotolewa si haba na zikisimamiwa vizuri zitaleta matokeo Chanya," alisema Mayeka.

Alishauri kampuni hiyo kuanzisha mashamba darasa kwenye maeneo ya wakulima ili kuwasaidia kuongeza ubora wa tumbaku inayozalishwa na kulifanya zao hilo kuwa endelevu.




Meneja Shughuli wa Kampuni ya Ununuzi wa Tumbaku ya Premium Active Tanzania, Nico Royssos (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 47.8 kwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, Mayeka Simon Mayeka wilayani humo jana, ambazo ni sehemu ya uchangiaji wa huduma za kijamii kwenye kata tisa za wilaya ya Chunya na Songwe ambazo zinazalisha tumbaku. **PICHA: NEBART MSOKWA**



## CCM yachangia ujenzi wa ofisi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimechangia mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya chama Kata ya Itezi jijini Mbeya ambayo ilianza kujengwa kwa nguvu za wanachama wa chama wa kata hiyo.

Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, Christopher Uhagile, alikabidhi saruji hiyo juzi kwa niaba ya chama na kuwapongeza wanachama kwa kusimamia vizuri mali za chama.

Pia, aliwapongeza wanachama kwa kuamua kujenga ofisi hiyo akisema miundombinu hiyo ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya chama katika eneo hilo.

"Yametajwa maeneo mengi hapa yanayomilikiwa na chama lakini maeneo haya yapo kwa sababu ya uzalendo wenu. Msingekuwa wazalendo haya maeneo yasingekuwapo," alisema Uhagile.

Alisema katika mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kata hiyo ya Itezi ndiyo itakuwa nzuri kuliko zote na kwamba eneo la ofisi hiyo ni kubwa kuliko maeneo mengine.

Diwani wa Itezi, Sambwee Shitambala, alisema eneo hilo lilikuwa limeuzwa kinyemela na wahuni na kwamba walitumia nguvu kubwa kulikomboa.

**Pia, aliwapongeza wanachama kwa kuamua kujenga ofisi hiyo akisema miundombinu hiyo ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya chama katika eneo hilo.**

# Ujenzi barabara kuleta mageuzi kiuchumi

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

UJENZI wa barabara ya Igwachanya - Itulahumba wilayani Wanging'ombe yenye urefu wa kilomita 19.25 kwa kiwango cha lami yenye thamani za Sh. bilioni 9.8, inataraji kuleta mageuzi kwa kuchochea fursa kwenye sekta ya kilimo pamoja na kufungua makao makuu ya wilaya baada ya kukamilika.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema hayo juzi wakati wa mkutano kwa kukabidhi mikataba ambayo Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) imeingia na kampuni ya Summer Communication Ltd pamoja na kumtambulisha mkandarasi huyo kwa wananchi.

Dk. Dugange alisema barabara hiyo ilikuwa kilio cha miaka mingi kwa wananchi kwa kuwa iliahidiwa miaka mingi lakini haikuwahi kutekelezwa.

"Kutoka Itulaumba kuja Igwachanya makao makuu ya wilaya yetu, tunakutana na tope wakati wa mvua. Tunakutana na vumbi wakati wa kiangazi kama sasa na mkaniambia Mheshimiwa Mbunge hii barabara itajengwa lini kwa kiwango cha lami? Nikawaambia naenda kumwomba Rais Samia (Suluhu Hassan) atupatie fedha tujenge barabara kiwango cha lami ili tufungue makao makuu ya wilaya yetu hapa Ingwachanya," alisema.

Dk. Dugange alimtaka mkandarasi wa barabara hiyo kuanza kazi mapema na kukamilisha kwa wakati ili kuleta tija kwa wananchi.

"Barabara hii ni mkombozi mkubwa kwetu. Itafungua uchumi wetu lakini mbali na barabara hii kuna kazi ya barabara inajengwa kutoka Igwachanya kwenda Ihanja na mimi mbunge wenu kupitia TARURA, TAMISEMI nilihakikisha tunapata bajeti nzuri sana wa ujenzi wa barabara zetu," alisema.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Njombe, Mhandisi Gerald Matindi, alisema Rais Samia ameendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kufungua barabara mkoani Njombe.

Vivian Mndolwa kutoka Summer Communication Ltd, alisema mradi wa Igwachanya -Itulahumba utekelezaji wake unatarajia kuchukua miezi 20.

Akisoma taarifa ya mradi huo, Meneja wa TARURA Wilaya ya Wanging'ombe, Boniface Kasambo, alisema barabara ya Igwachanya - Itulahumba ni miongozi mwa barabara zenye urefu wa kilomita 48.22 ambazo zinajengwa kwa kiwango cha lami kupitia programu ya Agri-Connect awamu ya pili nchi nzima.

# SMZ, GST kushirikiana utafiti wa kisayansi wa jiolojia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), kwa pamoja zimezindua ushirikiano wa kuanza utafiti wa kisayansi wa Jiolojia.

Hafla hiyo ilifanyika Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Maisara jana na taasisi hiyo itakuwa na kazi ya kufanya utafiti katika visiwa vya Zanzibar.

Meneja wa Jiolojia wa taasisi hiyo, Maswi Solomon, alisema taasisi hiyo, itakuwa Zanzibar kwa kushirikiana na wizara hiyo kuendesha utafiti wa kisayansi.

Alisema, watafanya utafiti utakaohusisha miamba kwa ajili ya kuchora ramani ya jiolojia ya visiwa vya Zanzibar, ambayo hivi sasa ramani hiyo haipo.

Alisema ramani ya jiolojia ni muhimu katika harakati za maisha na itahusisha kujua aina za miamba na aina ya madini yaliyopo Zanzibar.

"Hii itasaidia kujua miamba ambayo inaweza kuhifadhi maji, kutambua aina za mashimo hatarishi, pia kutambua baadhi ya viumbe na kujua hali ya udongo," alisema.

Alisema utafiti wa ramani ya jiolojia utakuwa unagusa maeneo mengi ikiwamo madini, ujenzi, kilimo, utalii, maafa na majanga na maji na itafanya kazi kwa lengo la kupata taarifa ili kuendelea ardhi.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Maji na Madini Joseph Kilangi, alisema hatua hiyo ni moja ya ushirikiano mzuri, baina ya Wizara ya Madini Zanzibar na ya Bara.

Alisema tukio hilo ni muhimu kwa kuwa wanaanza kazi ya utafiti wa miamba Zanzibar, kutengeza ramani kujua miamba yake.

Pia, serikali imepiga hatua kubwa kutokana na jambo hilo kutofanyika, lakini serikali ya awamu ya nane imethubutu kufanya hivyo na ramani ya Zanzibar kujulikana bahari pamoja na fukwe zake.

## Demokrasia Makini yahamasisha Wazanzibar kujiandikisha kupiga kura

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia Makini kimewaomba Wazanzibar wenye sifa, kujitokeza kuandikishwa katika daftari la kudumu la wapiga kura.

Kauli hiyo imetolewa jana na Katibu Mkuu wa chama hicho Ameir Hassan Ameir, wakati akizungumza na waandishi wa habari visiwani humo, kuhamasisha wananchi kutumia fursa ya kujiandisha katika daftari hilo.

Alisema Tume ya Uchaguzi Zanzibar imetoa taarifa ya kwa wananchi kuandikisha wapiga kura wapya, kuanzi mwezi Disemba kwani kufanya hivyo ni kutimiza matakwa ya sheria kama katiba ya Zanzibar inavyoelekeza, kuanzisha daftari la kudumu la wapiga kura na kuweka utaratibu wa kurekebisha yaliyomo katika daftari hilo.

"Ibara ya 8 (A) ya Katiba ya Zanzibar inaeleza kuwa mamlaka ya kuendesha nchi ni wananchi wenyewe, ambapo nguvu na mamlaka inatokana na wananchi wenywe," alisema.

Alisema ili kufikia malengo hayo, lazima wananchi wajitokeze kujiandikisha kupata nafasi ya kupiga kura, kutimiza matakwa yao ya kisheria, kwa kuwa wasipojiandikisha watakosa haki ya kuwachagua viongozi wanaowataka.

Aliwataka wazanzibar wote wenye vyama na wasio na vyama kujitokeza kujiandisha katika daftari hilo, hata asiye na chama ana haki ya kupiga kura kama atajiandisha mapema.

Pia, aliitaka ZEC kufuata sheria, kama kuna kasoro ndogo ndogo wazirekebishe ili kila mmoja apate haki yake.

Kuhusu masheha, alisema kwa mujibu wa sheria ni mawakala imeeleza wazi kuwa masheha, hawana mamlaka ya kumzuia mtu kujiandisha, wenye mamlaka ya kufanya hivyo ni Tume ya Uchaguzi kwa vigezo vilivyowekwa kisheria.

"Masheha wasiharibu daftari la wapiga kura, wasifanye kazi kwa mihemko ya kisiasa, wasiwakatae watu wenye sifa badala yake wafuate sheria ili kila mmoja apate haki yake," alisisitiza.

Aliwataka wananchi ambao hawana sifa ya kujiandikisha wahakikishe wahafiki katika vituo vya kujiandikisha, kwani endapo watakwenda wanaweza kusababisha fujo ambazo hazina msingi.




Ofisa Mauzo wa Kampuni ya Serengeti Breweries Ltd (SBL) Kanda ya Dar es Salaam Kusini, Doreen Tagalile (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. 500,000 kwa mshindi wa kampeni ya SBL Maokoto ndani ya Kizibo, Tumaini Ndumbaro, Savoy Lounge, eneo Buza, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoa msaada kisheria watakiwa kuendeleza jukumu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib Haji, amewataka watoa huduma za msaada wa kisheria kuendeleza jukumu la kutoa msaada wa kisheria kwa maslahi ya nchi.

Akizungumza jana wakati akifungua jukwaa la tatu la msaada wa kisheria kwa niaba yake, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Shaaban Ramadhan Abdalla, alisema serikali inatambua na kuthamini mchango wa wadau hao katika kuhakikisha jamii isiyo na uwezo inafikiwa vilivyo na kupata haki zao.

Alisema, watoa huduma hizo wakifikisha huduma za msaada wa kisheria ngazi ya jamii, walitumie jukwaa hilo katika kujadili, kubadilishana uzoefu, kuimarisha ushirikiano wa maswala ya msaada wa kisheria na kuendeleza juhudi za serikali kuhakikisha upatikanaji wa haki za jamii ya Wazanzibar.

Aidha, alifurahishwa na utekelezwaji wa maazimio yaliofikiwa na Idara ya Katiba na msaada wa kisheria kupitia utekelezaji wa jukwaa la pili la msaada wa kisheria na kuwataka katika jukwaa la tatu kuondoka na maazimio yatakayoimarisha masuala ya kisheria hasa katika mwelekeo wa mapitio ya sera ya msaada wa kisheria ya mwaka 2017 na kufana mabadiliko ya sheria ya msaada wa kisheria No. 13 ya mwaka 2018.

Mkurugenzi Idara ya Katiba na msaada wa kisheria, Hanifa Ramadhani Said, alisema lengo kuu la kufanyika kwa Jukwaa hilo ni kukuza ubunifu, kuimarisha ufanisi na weledi wa utendaji wa majukumu kwa watoaji wa msaada wa kisheria na kuwezesha upatikananji wa sera mpya zinazokidhi mahitaji ya jamii katika upatikanaji wa huduma za kisheria pamoja na kuwaunganisha watoaji wa msaada wa kisheria na taasisi nyingine ili kuwawezesha kufanya kazi kwa pamoja.

Mwakilishi wa Taasisi ya huduma za kisheria Tanzania (LFS), Wakili Alphonce Gura, alisema kwa sasa Zanzibar imekuwa sehemu ya kujifunza katika utoaji wa msaada wa kisheria kwa nchi za Afrika Mashariki hna taasisi hiyo itaendelea kuunga mkono jitihada hizo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Akifunga kongamano hilo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, aliagiza kufutwa kwa ada ya usajili kwa wasaidizi wa sheria kwasababu kazi wanayoifanya ni ya kujitolea.

Alisema, awali wasaidizi wa sheria walikua wakilipa Sh. 20,000 kwa mwaka kama ada ya usajili na kwa sasa ada hiyo imeondolewa rasmi.

Alizitaka taasisi zote zinazohusika na usimamizi wa sheria kushirikiana kwa pamoja kuimarisha maslahi ya wasaidizi wa sheria na kuwapongeza wasaidizi hao kwa kazi kubwa wanayoifanya bila ya malipo.

Katika Jukwaa hilo jumla ya maazimio tisa yamepitishwa na kuwasilishwa ripoti ya utekelezaji wake katika jukwaa linalofuata.

Miongoni mwa maazimio hayo ni kuhamasisha baadhi ya taasisi hususani vyama vya wafanyakazi kuwa na utaratibu wa kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa wanachama wake na kuweka wasaidizi wa sheria kwenye maeneo yao.

Vilevile, jukwaa limeazimia kwa Skuli ya Sheria Zanzibar kuweka ulazima kwa wanafunzi wanaosomea uwakili kutumia muda wa kutoa msaada wa kisheria kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo, pamoja na kuchapisha utafiti wa kitaifa kuhusu utoaji wa huduma za kisheria Zanzibar.



Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Kipunguni, jijini Dar es Salaam, Rozina Soka, akizungumza kwenye kikao cha kupanga mikakati ya kuhamasisha jamii ishiriki katika vita dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia, kilichoandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Tanzania yanadi leseni 441 za madini Uingereza

**LONDON, Uingereza**

WIZARA ya Madini imezinadi leseni zipatazo 441 za utafutaji wa madini muhimu na mkakati na leseni 46 kwa ajili ya uchimbaji wa madini hayo ambazo ni fursa kwa wawekezaji kwa ajili ya kuingia ubia na wamiliki wa leseni hizo kuziendeleza na hatimaye kuanzisha migodi.

Hayo yalibainishwa juzi na Kamishna Msaidizi wa Madini wa Wizara ya Madini, Ally Samaje, wakati akitoa wasilisho la wizara katika Siku ya kwanza ya Jukwaa la Biashara kati ya nchi ya Uingereza na Tanzania.

Aliieleza hadhira hiyo kuhusu madini muhimu na mkakati iliyopo Tanzania, fursa zilizopo katika uwekezaji kwenye madini hayo na mikakati ya serikali katika kuvutia uwekezaji.

Samaje alisema kati ya leseni hizo, Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) linayo miradi ya utafutaji madini muhimu ya lithium, graphite, rare earth elements na shaba ambayo iko katika hatua mbalimbali za uendelezaji na ambazo wawekezaji wanakaribishwa kushirikiana na STAMICO kuziendeleza kufikia hatua ya uchimbaji kwa manufaa ya pande zote mbili.

Mbali na miradi ya STAMICO, Samaje aliyataja baadhi ya madini muhimu na mkakati katika jukwaa hilo lenye lengo la kukuza ushirikiano wa kikanda na kuwavutia wawekezaji kuwekeza Tanzania katika sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya madini kuwa ni pamoja na madini ya lithium, graphite, iron, nickel, phosphate, rare earth element (REE), cobalt na shaba.

Aliongeza kwamba moja ya mikakati ya serikali katika kuendeleza madini muhimu nchini ni kupata taarifa za kina za kijiolojia kwa kufanya utafiti wa kina kwa kutumia ndege (High Resolution Airborne Geophysical Survey) mpaka kufikia takribani asilimia 50 ya ukubwa wa nchi ifikapo mwaka 2030, hatua ambayo itavutia uwekezaji Tanzania hususan katika hatua ya utafutaji madini mbalimbali.

"Hivi sasa utafiti wa aina hii nchini umefanyika kwa asilimia 16 tu. Hivyo, programu hii ni moja ya masuala muhimu yatakayotekelezwa kupitia 'Vision 2030 - Madini ni Maisha na utajiri'," alisema Samaje.

Alifafanua kuwa upatikanaji taarifa za kina za kijiolojia kupitia programu ya 'Vision 2030' kutasaidia kutambua maeneo yenye viashiria vya madini mbalimbali ili utafiti wa kina kama uchorongaji ufanyike katika maeneo hayo kwa lengo la kubainisha kuwapo mashapo ya madini yanayoweza kuchimbwa kibiashara.

"Upatikanaji wa taarifa za kijiolojia katika maeneo ya wachimbaji wadogo utasaidia wachimbaji kwa tija bila kupoteza mitaji yao.

"Pia taarifa zitakazopatikana zitatumiwa na wizara na taasisi nyingine za serikali kama vile Wizara ya Maji kujua maeneo yenye miamba yenye mikondo ya maji chini ya ardhi kwa matumizi mbalimbali," alifafanua.

Jukwaa hilo limeandaliwa na Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Ubalozi wa Uingereza Tanzania.

Sekta za umma kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar zinazoshiriki katika jukwaa hilo ni pamoja na viwanda, kilimo, madini, nishati, uchumi wa buluu, fedha, uwekezaji na biashara.

Sekta ya Madini, ujumbe wake unaongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara, Kheri Mahimbali, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), Dk. Mussa Budeba, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Augustine Olal, Kamishna Msaidizi wa Madini, Samaje na Mchumi, Aman Ng'oma.

## Chuo cha Kodi chaanza kufundisha kodi kidijitali

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Kodi (ITA) kimeanza kutoa mafunzo kwa njia ya mtandao, kikiwavutia Watanzania wengi kusomea masomo ya uhasibu na kodi.

Jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Isaya Jairo, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mahafali ya 16 ya chuo hicho.

Alisema kuwa wao ni chuo pekee nchini na katika Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika chenye usajili na ithibati ya kudumu kutoa mafunzo ya forodha na kodi kwa wadau mbalimbali katika ngazi ya shahada ya awali na shahada ya uzamili.

Alisema chuo hicho kimekuwa kinatoa mafunzo yanayoendana na mabadiliko ya sayansi, teknolojia na uchumi yanayolenga mahitaji ya soko la wataalamu wanaohitajika katika nyanja za forodha na kodi nchini, barani Afrika na ulimwenguni.

Alisema kwa kuzingatia uhusiano na ushirikiano uliopo kati ya chuo na mamlaka za mapato za Afrika, kimewaalika baadhi ya wakuu wa mamlaka za mapato mbalimbali ambapo tayari baadhi ikiwamo Uganda wamethibitisha kushiriki.

Alisema mahafali ya 16 yanafanyika wakati chuo hicho kinajivunia mafanikio mengi katika utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Tano wa Chuo ambao umejikita zaidi katika kutoa mafunzo kwa njia ya kisasa za kidijitali.

"Chuo cha Kodi ambacho ni sehemu ya Mamlaka ya Mapato (TRA) pia kinatoa ushauri na kuwajengea uwezo watumishi wa TRA, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na mamlaka zingine za mapato Afrika," alisema.

Kiongozi huyo alisema mahafali ya 16 yatafanyika kesho. Wahitimu 508 wanatarajiwa kutunukiwa vyeti. Kati yao, wahitimu 293 ni wanaume na 215 ni wanawake.

KUPOTEA KWA VYETI



**CHRISTIAN LUKALI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S8003/0134 kilichotolewa Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST. MATTHEW SEKONDARI mwaka 2005. Cheti cha chuo cha Ualimu chenye namba E514/0233 kilichotolewa na CHUO CHA UALIMU ILONGA mwaka 2008. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:
**PHQ/DAR/KIN/4250/2023.**

KUPOTEA KWA HATI YAKUSAFIRIA



**JULIETH GEORGE WILLIAM,** Anatangaza kupotea kwa Hati yakusafiria yenye namba **TAE 599868** iliyotolewa makao makuu Mwaka 2023. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/9590/2023.**

KUPOTEA KWA CHETI CHA USAJIRI WA MSKITI WA MASJID HUDAA-CHAMWINO MJINI

MOHAMED JUMA HASSAN KATIBU WA MASJID HUDAA, Anatangaza kupotea kwa Cheti cha Usajiri wa Mskiti wa Masjid Hudaa kilichotolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: PHQ/DOD/DOD/9534/2023

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SINGIDA LILILOPO SINGIDA

SHAURI LA MAOMBI YA ARDHI NA. 76 YA 2023

MUSA YUSUFU MUSA.........................MWOMBAJI

DHIDI YA

GERALD ZEPHERINE.....................MJIBU MAOMBI

KWA: GERALD ZEPHERINE – POPOTE ULIPO TANZANIA

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa mwombaji tajwa hapo juu ameleta maombi yake hapa Barazani ambayo maelekezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi, ambayo yanaweza kupatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria hapa Barazani tarehe 24/11/2023 saa 2:00 asubuhi siku ya kutajwa kwa shauri hilo. Unatakiwa uhudhurie mwenyewe au mwakilishi wako anaetambuliwa kisheria siku na saa tajwa hapo juu.
**ANGALIA:** Kushindwa au kupuuza kufika tarehe na saa iliyotajwa hapo juu kesi itapangwa na kusikilizwa upande mmoja tu na uamuzi kutolewa bila ya wewe au mwakilishi wako kuwepo.

HATI hii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya BARAZA hii leo tarehe 06 Mwezi wa Novemba, Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA SINGIDA.
CHAIRMAN DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL SINGIDA TANZANIA

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ODILO KAPIS TWEVE**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari (Toyota-Landcruiser) yenye namba za usajili **T 968 ALW,** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**PHQ/MOR/MOR/6493/2023.**

## HABARI KIMATAIFA

# Mashambulizi yaongezeka Israel wakati usitishwaji vita ukikaribia

**GAZA,** PALESTINA

JESHI la Israel (IDF) liliendelea kufanya mashambulizi makali kutoka angani, ardhini na baharini katika maeneo mbalimbali ya Ukanda wa Gaza jana.

Mashambuli hayo yalifanyika kabla ya muda wa kusimamisha mapigano kati ya wanamgambo wa Hamas na Jeshi la Israel kwa ajili ya kubadilishana mateka.

Kutokana na taarifa katika eneo la mapambano, mashambulizi yaliongezeka zaidi katika saa za mwisho kabla ya kufikia usitishaji mapigano, huku ndege za Israel zilitupa mabomu katika maeneo tofauti ya Ukanda wa Gaza.

Kufuatia mashambulizi hayo, Wapalestina kadhaa waliuawa na wengine kujeruhiwa wengi wao wakiwa raia.

Idadi ya waathiriwa wa uvamizi wa Israel mjini Gaza tangu kuanza kwa uvamizi huo siku 47 zilizopita imeongezeka.

Hadi sasa jumla ya watu 14,128 wamefariki wakiwamo watoto zaidi ya 5,840 na wanawake 3,920, kulingana na Wizara ya Afya ya Palestina na idadi ya waliojeruhiwa iliongezeka hadi 33,000 waliojeruhiwa.

Israel na Hamas zimekubaliana kusitisha mapigano kabisa kwa siku nne ambapo mamia ya malori zilizosheheni misaada ya kibinadamu na mafuta yataruhusiwa kuingia Gaza, na ofisa wa Marekani alisema kuwa mpango huo ni hatua kuelekea kuachiliwa kwa mateka zaidi.

Kundi la kwanza la mateka linatarajiwa kuachiliwa Alhamisi - siku ya kwanza ya utekelezwaji wa makubaliano ya usitishaji mapigano.

Wakati wa kuanza kwa usitishwaji wa vita unastahili kutangazwa katika saa 24 zijazo.

Katika taarifa lililotumwa katika mtandao wa X, zamani Twitter, IDF ilitoa maelezo ya mashambulizi ya ndege, kufyatuliana risasi na wapiganaji wa Hamas na uharibifu wa miundombinu inayodaiwa kuwa ya Hamas.

Maeneo yaliyolengwa ni pamoja na Khan Younis, mji ambao uko kusini mwa Ukanda wa Gaza.

Maafikiano yaliyofikiwa kati ya pande zote mbili ni usitishwaji wa mapigano kwa siku nne na ilitarajiwa kutangazwa jana.

Picha za anga zilizochukuliwa Gaza asubuhi ya jana zinaonyesha moshi ukipaa juu ya eneo hilo baada ya shambulio la anga la Israel.

Wakati huo huo, Israel imetoa orodha ya Wapalestina 300 ambao wanaweza kutolewa chini ya makubaliano yaliyofikiwa kati ya Israel na Hamas.

Orodha hiyo, iliyowekwa kwenye tovuti ya Wizara ya Sheria ya Israel, inajumuisha majina ya wahusika, umri na makosa yaliyosababisha kushikiliwa.

Kati ya hao, wafungwa 150 pekee ndio wanaotarajiwa kuachiliwa katika makubaliano hayo, huku Hamas wakiwaachia mateka 50 wa Israel.

Marekani pia imethibitisha kwamba zaidi ya idadi hiyo ya mateka watakaoachiliwa kutoka kwenye mikono ya Hamas.

Ofisa mmoja wa Wizara ya Mambo ya Nje, alisema mpango huo ulivyopangwa ndivyo unavyohimiza kuachiliwa kwa kila mtu.

Katika hatua nyingine, wabunge wa Afrika Kusini wamepiga kura ya kuufunga ubalozi wa Israel mjini Pretoria na kusitisha uhusiano wa kidiplomasia.

Chama tawala cha African National Congress (ANC) ambacho kinatawala bunge kimekuwa kikiikosoa Israel kwa muda mrefu na kuongoza upigaji kura hiyo bungeni.

Hoja hiyo ilitoa wito wa kufungwa kwa ubalozi huo na kusitishwa kwa uhusiano hadi Israel itakapokubali kusitisha mapigano na kufanya mazungumzo ya Amani.

Hoja hiyo ilipitishwa kwa kura 248 dhidi ya 91 na kusababisha wabunge kupiga kelele za “Palestina huru, huru”.

Kabla ya upigaji kura, Israel ilimwita balozi wake kwa mashauriano hatua ambayo ilisema ilitokana na taarifa za kura hiyo.

Rais Cyril Ramaphosa hivi karibuni aliishtaki Israel kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kwa uhalifu wa kivita.

Wakati akiongoza mkutano wa kilele wa kundi la nchi za Brics siku ya Jumanne kujadili hali ya Gaza, Ramaphosa lugha yake ilikuwa kali, akiishutumu Israel kwa kufanya mauaji ya halaiki huko Gaza na pia kukemea kile alichokiita adhabu ya pamoja ya raia wa Palestina.



Wingu la moshi ulioambatana na moto uliotokana na bomu lililorushwa na ndege ya Israel katika eneo la gaza jana asubuhi. **PICHA: REUTERS**

## Guterres alaani Korea Kaskazini kurusha satelaiti mzingo wa dunia

**NEWYORK,** MAREKANI

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, amelaani hatua ya Korea Kaskazini ya kurusha satelaiti ya upelelezi katika mzingo wa dunia.

Msemaji wa Katibu Mkuu huyo, Farhan Haq, alieleza kuwa kiongozi huyo amelaani vikali kurushwa kwa satelaiti ya kijeshi ya nchi hiyo kwa kutumia teknolojia ya makombora ya balistiki.

Haq aliongeza kuwa, urushwaji wa satelaiti hiyo ya kijasusi katika mzingo wa dunia unakwenda kinyume na maazimio ya baraza la usalama la Umoja wa Mataifa.

Hilo ni jaribio la tatu la Korea Kaskazini la kurusha satelaiti katika mzingo wa dunia, baada ya majaribio mawili ya awali kufeli.



# Mose Katumbi azidi kuungwa mkono DRC

**KINSHASA, DRC**

KINARA wa upinzani katika uchaguzi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambaye alikuwa gavana wa Katanga, Moise Katumbi, anaendelea kufanya kampenzi zake kwa mafanikio baada ya wagombea zaidi wa kiti cha urais kujitoa na kuhamia kambi yake.

Katumbi alianza safari ya kuwania nafasi hiyo kaskazini mwa mji wa Kisangani.

Awali Waziri Mkuu wa zamani, Matata Ponyo, alikuwa wa kwanza kujiondoa katika orodha ya mgombea na kutangaza kumuunga mkono Katumbi. Wagombea wengine waliotia nia kutangaza kuwa na Katumbi ni Seth Kikuni na Frank Diongo.

Wagombea wengine waliozindua kampeni zao kutaka kumwondoa madarakani Rais Filex Tshisekedi ni Daktari Denis Mukwege na mwanamke pekee kwenye kinyang'anyiro hicho, Marie-Josee Ifoku.

Rais wa sasa Felix Tshisekedi anayewania kuchaguliwa kwa muhula wa pili, alizindua kampeni jijini Kinshasa kwenye uwanja wa Martyrs na kuahidi kukamilisha ahadi za uchaguzi na kusimamia usalama mashariki mwa nchi hiyo.

Mgombea mwingine wa upinzani ambaye anaonekana kuwa tishio kwa Tshesekedi ni Martin Fayulu, ambaye katika kampeni zake ameahidi atashughulikia changamoto zinazoikabili nchi hiyo kwa sasa.

# AZAM, DODOMA JIJI VINARA U-20, YANGA YASHIKA MKIA

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za vijana za Azam FC na Dodoma Jiji zinaongoza katika Ligi ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (U-20), inayondelea hapa nchini wakati Simba ikiwa hoi huku Yanga ikiburuza mkia.

Wakati Azam ikiongoza Kundi A, Dodoma Jiji inaongoza Kundi B katika ligi hiyo inayofanyika kwenye viwanja mbalimbali nchini, ikiwa imeingia katika raundi ya nne.

Kwa mujibu wa msimamo uliotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), jana, Azam inaongoza ikiwa na pointi tisa, kwa kucheza mechi nne, ikishinda tatu na kupoteza moja, ikifuatiwa na Coastal Union yenye pointi nane, iliyocheza mechi nne, kushinda mbili na sare mbili, Prisons ikishika nafasi ya tatu ikiwa ina pointi saba ilizozipata kwa kucheza mechi nne, ikishinda mbili, sare moja na kupoteza moja.

Namungo ipo nafasi ya nne ikiwa na pointi nne, Simba ya tano ikiwa na pointi tatu, Ihefu inashika nafasi ya sita ikiwa na pointi tatu pia, KMC ya saba na pointi zake mbili, huku timu ya Yanga chini ya miaka 20 ikiburuza mkia ikiwa na pointi mbili mpaka sasa ikiwa na pointi mbili.

Kundi B linaongozwa na Dodoma Jiji FC ambayo imejizolea pointi 12 mpaka sasa baada ua kushinda mechi zote nne ilizocheza huku Mtibwa Sugar ipo nafasi ya pili ikiwa na pointi saba na mabao 11, Singida Fountain Gate nafasi ya tatu ikiwa na pointi saba na mabao sita, nafasi ya nne ikichukuliwa na JKT Tanzania ikiwa pia na pointi saba, lakini imefunga matatu.

Geita Gold inakamata nafasi ya tano na pointi zake sita, Mashujaa FC ipo nafasi ya sita pointi zake tatu, Tabora United nafasi ya saba ikiwa na pointi mbili, Kagera Sugar ikiburuza mkia ikivuna pointi moja tu katika mechi nne ilizocheza.

Ligi hiyo inashirikisha timu za vijana za klabu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo bingwa wake mtetezi ni Yanga ya Dar es Salaam.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Vijana ya Wanaume ya umri chini ya miaka 18 wakifanya mazoezi kujiandaa na michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-18), itakayofanyika kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 9, mwaka huu katika vituo viwili vya Kisumu na Kakamega, Kenya. **PICHA: TFF**

# Wanariadha wanawake darasani

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limeandaa kongamano la wanawake maalum kwa ajili ya mchezo wa riadha litakalofanyika kuanzia leo kwenye viwanja vya Uhuru na Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mtendaji wa BMT, Neema Msitha, alisema kongamano hilo ambalo hufanyika kila mwaka litakuwa la siku tatu na litahusisha wanariadha wanawake.

Msitha alisema siku ya kwanza ya kongamano kutakuwa na wakufunzi mbalimbali ambao watatoa elimu ya ujasiriamali ili kuwawezesha wanawake kujiandaa na maisha baada ya michezo.

"Pia semina ya uongozi namna gani anaweza kujisimamia hapo baadaye watakapoachana na mchezo huu na kupata nafasi katika kuongoza katika sehemu nyingine ikiwamo kuchaguliwa katika vyama vya michezo.

Mgeni rasmi atakaye hudhuria siku ya mwisho ambaye tunamtarajia ni Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro," alisema Msitha.

Mwakilishi wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Michael Washa, alisema mashindano hayo yatashirikisha mikoa 31 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

"Mpaka sasa mikoa 25 imethibitisha kushiriki mashindano hayo huku mikoa mingine sita ikiendelea na taratibu za kujisajili wakati michezo sita itashindaniwa ikiwamo kurusha mkuki, kupokezana vijiti na mbio za mita 100, 200, 2000, 1000, 800, 1500 na 5000.

## Ainembabazi, Wambui watua Simba Queens

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumtangaza winga kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Isabelle Diakiese na kiungo mshambuliaji, Mganda Riticia Nabbosa, kutoka Fountain Gate Princess, Simba Queens imeendelea kujiimarisha kwa kuwasajili, Joanita Ainembabazi na beki wa kati, Elizabeth Wambui.

Joanita anayeichezea Timu ya Taifa ya wanawake ya Uganda na Wambui yupo katika kikosi cha She Starlets.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mussa Hassan Mgosi amesema jana usajili walioufanya ni kutaka kurejesha makali ambayo timu hiyo ilikuwa nayo misimu miwili iliyopita ambapo walitwaa ubingwa wa Tanzania Bara, Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) na kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita.

"Tumesajili kwa ajili ya kutaka kuziba zile nafasi ambazo zilionekana zina mapungufu katika msimu uliopita, tunataka kurejesha heshima yetu kwa sababu tuna malengo makubwa hasa katika mechi za kimataifa," alisema Mgosi.

## JKT TZ yajiimarisha kuwakabili Ihefu SC

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha inaondoka na pointi tatu, JKT Tanzania imeandaa programu maalumu ya mazoezi kwa ajili ya kuwavaa Ihefu SC katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msemaji wa JKT Tanzania, Masau Bwire. alisema wachezaji wote wana morali ya juu kuelekea mechi hiyo.

"Kila mchezo kwetu ni sawa na fainali, tunaipambania timu yetu kuhakikisha inafanya vyema katika mechi hii ijayo kwa sababu tunaamini mchezo huo utakuwa na upinzani mkubwa, " alisema Bwire.

Aliongeza wanaipa umuhimu mkubwa mchezo huo kwa sababu wanatambua msimu huu kila timu imejipanga vizuri ili kuvuna pointi mapema na kujinusuru na janga la kushuka daraja.

"Tunafahamu Ihefu ni timu nzuri, hivyo tutaingia uwanjani kwa tahadhari tukiwa na lengo la kupata matokeo mazuri, kila mchezaji wetu anajua hakuna mechi rahisi kwenye ligi hii, pia tunawaomba mashabiki wetu waendelee kutuunga mkono," Bwire alisema.

## ZISIKUPITE

### NEVES KUTUA CITY
BERNADO Silva amedokeza anaweza kujaribu kumshawishi, Joao Neves, mwenye umri wa miaka 19 ajiunge na Manchester City licha ya Manchester United kumtaka kiungo huyo wa Benfica. **(MEN)**

### RUBEN HAONDOKI SAUDIA
KIUNGO wa kati wa Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 26, hatarajiwi kuondoka katika klabu ya Saudia ya Al-Hilal ifikapo Januari kutokana na kuhusishwa na Newcastle United**. (Mail)**

### SILVA KUREJEA BENFICA
KIUNGO wa kati wa Manchester City na Ureno, Bernado Silva mwenye umri wa miaka 29 amesema angependa kurejea kuichezea Benfica kabla ya kumaliza soka yake. **(CNN, via TalkSport)**

### VARANE KUBAKIA UNITED
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, hatamruhusu mlinzi wa kati Mfaransa Raphael Varane mwenye umri wa miaka 30 kuondoka katika klabu hiyo hadi dirisha la usajili la majira ya joto. **(Sun)**

### JUVE YAMTAJA VLAHOVIC
KLABU ya Juventus ina matumaini mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 23 atakubali kusaini mkataba wa nyongeza katika timu hiyo licha ya kutakiwa na Arsenal na Manchester United. **(90min)**

### ROMA KUMBAKIZA LUKAKU
CHELSEA ina matumaini itaweza kumuuza mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku msimu ujao wa joto, huku AS Roma ikitamani kufanya uhamisho wa mkopo wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kuwa wa kudumu. **(Evening Standard)**

### GRIEZMANN AIKATAA UNITED
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Antoine Griezmann hatajiunga na Manchester United na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 analenga kubakia Atletico Madrid. **(Fabrizio Romano)**

### PALHINHA KUTUA BAYERN
FULHAM itamruhusu kiungo wa kati wa Ureno, Joao Palhinha, mwenye umri wa miaka 28 kuondoka na kujiunga na Bayern Munich Januari kwa dau la chini ya euro 60 ambayo klabu ilitaka hapo awali. **(Florian Plettenberg, Sky Germany)**

### DE GEA KWENDA MAREKANI
GOLIKIPA wa Hispania, David de Gea ameweka wazi hataki kujiunga na klabu ya Saudia, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 anaweza kuhamia Ligi Kuu ya Soka ya Marekani hapo mwakani. **(90min)**

### TOMIYASU ANUKIA BAYERN
KLABU ya Bayern Munich inashinikiza kumsajili beki wa Japan, Takehiro Tomiyasu, msimu ujao wa joto, lakini Arsenal hawataki kumwachia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. **(Florian Plettenberg, Sky Germany)**

### NYOTA UNITED WAFUNGUKA
BAADHI ya wachezaji wa Manchester United wanaamini mwanzo mbaya wa timu hiyo msimu huu ulisababishwa na kocha Erik ten Hag kukifanyisha kikosi kazi kupita kiasi katika maandalizi ya msimu mpya. **(Guardian)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MIAMI YAGOMA MESSI KUKUTANA NA RONALDO

●●●Ni katika michuano ya Kombe la Riyadh ambayo itafanyika...

**MIAMI, Marekani**

KLABU ya Inter Miami imekanusha ilikubali kushiriki katika mechi ya kirafiki ya Kombe la Riyadh itakayofanyika Februari, mwakani dhidi ya Al Nassr, ambao ungeweza kumshuhudia Lionel Messi akichuana na mpinzani mkubwa, Cristiano Ronaldo kwa mara ya mwisho.

Waandaaji wa mchezo huo nchini Saudi Arabia walikuwa wametangaza tukio la "Ngoma ya Mwisho" kupitia mitandao ya kijamii kwenye Ukumbi wa Kingdom Arena mjini Riyadh bila kuweka tarehe kamili.

Hata hivyo, Miami ilisema baadaye hakuna makubaliano yaliyofikiwa.

"Tumesikia tangazo lilitolewa ikisema Inter Miami CF imeratibiwa kucheza Kombe la Msimu wa Riyadh. Hii sio sahihi," Idara ya mawasiliano ya Inter Miami CF ilisema katika taarifa.

"Toleo hilo lilijumuisha taarifa zinazohusishwa na mmiliki wa timu, Jorge Mas. Mas hajatoa maoni yoyote hadharani au kwa faragha, kuhusiana na ziara ya maandalizi ya msimu mpya.

"Tangu siku ya kwanza, Inter Miami CF imejipanga chapa ya kimataifa. Kwa ajili hiyo, tumekuwa kwenye mazungumzo ili kubainisha ratiba yetu ya msimu wa kabla ya msimu wa 2024. Tunatazamia kuwaonyesha wachezaji wetu kwenye ziara ya kwanza ya kimataifa ya Inter Miami CF ambayo itatangazwa katika wiki zijazo."

Tangazo la awali lilisema mchuano huo wa timu tatu utakamilika na Al Hilal ya Neymar, ingawa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil ni majeruhi.

"Msisimko na shauku ya kimataifa ambayo tunatarajia kuibua mashindano haya inaongezeka juu ya moja ya matarajio yetu kuu ya msimu wa Riyadh -- kuunda hafla za kimataifa ambazo wageni wa Riyadh na mashabiki kote ulimwenguni wanaweza kufurahia," alisema Turki Alalshikh, Mwenyekiti wa Mamlaka Kuu ya Burudani ya Saudia.

Saudi Arabia imefanya msukumo mkubwa katika soka la dunia kwa kusajili baadhi ya wachezaji wakubwa wa mchezo huo.

Lakini haikuweza kumvutia Messi kwenye ufalme huo tajiri kwa mafuta alipoondoka Paris Saint-Germain mwishoni mwa msimu uliopita, huku mshindi huyo mara nane wa Ballon d'Or akiamua kuhamia Ligi ya Soka ya Marekani (MLS), badala yake.

Mara ya mwisho kwa wapinzani hao wawili wa LaLiga kucheza dhidi ya kila mmoja ilikuwa Januari 19, 2023, mjini Riyadh.

Messi alishiriki Kombe la Msimu wa Riyadh msimu uliopita akiwa na PSG na pia akaja dhidi ya Ronaldo baada ya nyota huyo wa Ureno kuhamia Al Nassr. PSG ilishinda kwa mabao 5-4.

Mei, mwaka huu Messi alipigwa faini na kusimamishwa na klabu hiyo ya Ufaransa kwa safari isiyoidhinishwa kwenda Saudi Arabia.

Messi, ambaye aliiongoza Argentina kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia mwaka jana, tayari ameshinda kombe lake la kwanza akiwa na Miami.

Messi na Ronaldo wanachukuliwa wachezaji wawili wazuri bora zaidi wa wakati wote na walishindana kila mmoja kwa tuzo kubwa zaidi za soka wakati wa miaka yao nchini Hispania katika klabu za Barcelona na Real Madrid.

# SCALONI: NAFIKIRIA KUONDOKA ARGENTINA



**RIO DE JANEIRO, Brazil**

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Scaloni, amesema kwa sasa anajiuliza kama abakie kuendelea kukinoa kikosi hicho ama la, imeelezwa.

Scaloni alitoa dokezo hili baada ya Argentina kuifunga Brazil bao 1-0 katika mchezo wa kufuzu michuano ya Kombe la Dunia 2026, usiku wa kuamkia jana.

"Nahitaji kufikiria sana nitakachofanya," alisema Scaloni katika mkutano na waandishi wa habari baada ya ushindi huo dhidi ya Brazil mjini Rio de Janeiro.

"Nahitaji wakati huu kufikiria."Scaloni alisema angefikiria kabla ya kuzungumza na Rais wa Shirikisho la Soka la Argentina, Claudio Tapia, na wachezaji "kwa sababu timu hii ya taifa inahitaji kocha ambaye ana kila nguvu iwezekanayo, na anajisikia vizuri."

Matokeo hayo kwenye Uwanja wa Maracana yalikuwa ni mechi ya kwanza kabisa kwa Brazil kushindwa nyumbani katika mechi ya kufuzu Kombe la Dunia.

"Si kwaheri, si kitu kingine. Lakini ninahitaji kufikiria kwa sababu ari ipo juu sana na ni ngumu kuendelea," alisema Scaloni. "Ni vigumu kuendelea kushinda."

Hakujibu maswali mengine baada ya kutoa maoni yake.

Scaloni (45), ambaye mkataba wake uliongezwa hadi Kombe la Dunia la 2026 baada ya ushindi wake mwaka jana nchini Qatar, alichukua nafasi ya Jorge Sampaoli baada ya Argentina kufungwa na Ufaransa katika hatua ya 16 bora kwenye fainali za Kombe la Dunia la mwaka, 2018.

Kabla ya kuhudhuria mkutano wa wanahabari Jumanne, Scaloni alionekana akiwakumbatia na kuwabusu wahudumu wengine wa Argentina. Ilikuwa mechi ya mwisho ya timu hiyo kwa mwaka 2023.

Argentina inaongoza mchuano huo wa timu 10 wa kufuzu kutoka Amerika Kusini ikiwa na pointi 15 katika mechi sita, ikifuatiwa na Uruguay yenye pointi 13 na Colombia 12. Brazil ipo nafasi ya sita, ikiwa na pointi saba.

Kombe la Dunia la 2026 litafanyika nchini Marekani, Mexico na Canada litajumuisha timu 48, ikimaanisha kuingia moja kwa moja kwa timu sita kutoka Amerika Kusini.

# Havertz afunguka alivyotua Arsenal




**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Kai Havertz amekiri kupata ugumu wa kujiunga na klabu hiyo kutoka kwa mahasimu wao wa jiji la London, Chelsea, akisema bado hajaaminiwa na mashabiki.

Havertz alijiunga na Arsenal kwa uhamisho wa pauni milioni 65 baada ya kuhangaika kupata kiwango chake kwa uhamisho wake wa pauni milioni 71 kwenda Chelsea kutoka Bayer Leverkusen miaka mitatu iliyopita.

Tangu ahamie London, Havertz bado hajawa katika kiwango chake ambacho kilimfanya kuwa miongoni mwa vijana wenye vipaji vya kutumainiwa barani Ulaya, huku Kocha, Mikel Arteta akijaribu kumchukua mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani kwenye kikosi chake.

Licha ya ugumu wake, Havertz amesisitiza anafurahi kuwa Arsenal.

"Kutoka nje, Arsenal siku zote ilionekana kama familia," alisema akiiambia tovuti rasmi ya klabu hiyo.

"Hiyo ndiyo hisia niliyokuwa nayo wakati nikicheza. Na nilipojiunga, ndivyo ilivyokuwa, na wafanyakazi ni wazuri pia - na hiyo hurahisisha maisha kwa mchezaji mpya.

"Tangu dakika ya kwanza nilipozungumza na Mikel (Arteta) kuhusu kujiunga na Arsenal, nilikuwa na hisia kwamba anatuheshimu sana sote, kwa hiyo hiyo ilikuwa sehemu kubwa ya mimi kujiunga na klabu. Nilihisi tu umoja wa klabu kutoka kwa wachezaji na hasa ndani ya mashabiki na klabu nzima.

"Ni muhimu sana kuaminiwa na mashabiki. Siku zote ni ngumu unapotokea Chelsea, kwa sababu ni wapinzani wakubwa, hivyo inaweza kuchukua wiki kadhaa kupata imani kutoka kwa mashabiki.

"Lakini mabao na michezo mizuri inaweza kunisaidia na siku zote nitatoa asilimia 100 katika michezo na vipindi vya mazoezi. Nadhani watalitambua hili pia, ambalo ni muhimu sana. Nina furaha sana kuwa hapa."

## Guardiola kocha mwenye ushawishi zaidi

**LONDON, England**

PEP Guardiola ametawazwa kuwa kocha mwenye ushawishi mkubwa zaidi katika soka la England kutokana na ripoti ya LiveScore baada ya kupigiwa kura nyingi na watumiaji wa mtandao huo ijulikanayo 'Mageuzi ya Mashabiki'.

Ligi Kuu England inaanza tena wikendi hii huku Manchester City ya Guardiola ikiwakaribisha Liverpool mechi itakayochezwa Jumamosi.

Na ingawa pambano la uwanjani linaonekana kuwa gumu, watumiaji wa LiveScore wamempigia kura kocha huyo wa City kama kocha mwenye ushawishi zaidi na kuwabwaga, Sir Alex Ferguson na Jurgen Klopp.

Katika kura hizo asilimia 52 walimchagua Guardiola dhidi ya makocha hao wawili.

Huku asilimia 50 wakimpigia kocha mkuu wa zamani wa Manchester United, Ferguson na asilimia 32 walimchagua Klopp.

Kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 25 ya LiveScore, ripoti ya Mageuzi ya Mashabiki huchanganua data kutoka kwa karibu watumiaji 25,000 wa programu za Uingereza na kufichua mabadiliko ya tabia za mashabiki wa soka katika kipindi chote hicho.

Kwa kuwa ripoti inapaswa kutolewa kikamilifu mwanzoni mwa 2024, wasomaji wanaweza kutazamia maarifa mengi ya kuvutia kutoka kwa data iliyokusanywa.



## HABARI MICHEZO

# ROTARY YAANDAA NUSU MARATHON KUTIBU MACHO

**Na Beatrice Shayo**

KLABU ya Rotary eClub-Masaki ya jijini Dar es Salaam imezindua mbio za nusu marathon kwa ajili ya kuchangisha fedha za kusaidia kutoa mitababu ya macho.

Mbio hizo zilizopewa jina la 'Run for Sight, zitafanyika Januari 12 mwakani na kujumuisha zaidi ya washiriki 2,000 ambao watachangia fedha kwa ajili ya kusaidia watu wenye matatizo ya macho.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Rais wa klabu hiyo, Leena Kapadia, alisema wanatarajia kukusanya Shilingi milioni 70 zitakazosaidia kutoa matibabu ya macho kwa wananchi wenye uhitaji.

"Kupitia mbio hizi tunalenga kuleta mabadiliko katika maisha ya wale wenye matatizo ya macho nchini. Fedha zitakazopatikana zitasaidia kuweka kambi ya matibabu ya macho pamoja na kufanya upasuaji bila malipo na huduma muhimu za wenye matatizo hayo," alisema Kapadia.

Alisema waliamua kufanya mbio hizo kwa sababu takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonyesha takribani watu bilioni moja, wana matatizo ya kuona na wengi wao wanaishi kwenye nchi zinazoendelea kama Tanzania.

Aidha, Mratibu wa mbio hizo, Reshma Shah, alisema mwaka jana waliendesha mbio kama hizo na washiriki 1,283 walikimbia na kukusanya Sh. milioni 14 ambazo ziliendesha kambi ya matibabu ya macho katika mikoa ya Kahama, Mwanza na Zanzibar.

Alisema jumla ya wagonjwa 9,027 walipimwa huku 587 wakifanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho bila malipo na sasa wamerudi tena ambapo Januari 12 mwakani watakusanya fedha hizo kwa ajili ya kambi ya matibabu.

Alisema katika mbio hizo kila mshiriki atachangia Sh. 35,000 ambapo washindi watapewa zawadi mbalimbali ikiwamo fedha kuanzia Sh. milioni 1.5 kwa mshindi wa kwanza, Sh. 750,000 mshindi wa pili na Sh. 500,000 kwa mshindi wa tatu.

"Mbio hizi ni tukio muhimu na fedha zitakazopatikana zitasaidia upasuaji wa mtoto wa jicho, upasuaji mdogo, kutibu upungufu wa seli unaosababishwa na uzee, trakoma na matatizo mengine yatokanayo na ugonjwa wa macho," alisema.




Msemaji wa shindano jipya la 'Magift Dabo Dabo', Haji Manara (kushoto) akizungumza na Waandishi wa Habari juu ya Shindano hilo jipya, pembeni ni Ofisa Mkuu wa Tigopesa, Angelica Pesha. **PICHA:MPIGA PICHA WETU**

# Tigo yaja na shindano jipya

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu ya Tigo jana imezindua shindano lake jipya kwa ajili ya wateja wake ambapo zawadi mbalimbali zitatolewa yakiwamo magari mawili mapya.

Shindano hilo lililopewa jina la 'Giftisha dabo dabo' litamwezesha mteja wa kampuni hiyo kushinda zawadi pamoja na mpendwa wake atakayemchagua.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam kwenye hafla fupi ya kuzindua shindano hilo, Mkurugenzi wa Masoko wa Tigo, Edwardina Mgendi, alisema kampuni hiyo itatumia mpaka Shilingi milioni 165 kama zawadi wakiwa na lengo la kuwapongeza wateja wao, lakini kuwazawadia kwa kuwa nao pamoja kwa mwaka mzima.

"Hili ni shindano ambalo wateja wetu watapata fursa ya kushinda zawadi mbalimbali na kuwapa nafasi pia wapendwa wao kushinda, tunataka kufurahi pamoja na wateja wetu," alisema Mgendi.

Aidha, Ofisa Mkuu wa TigoPesa wa Kampuni hiyo, Angelica Pesha, alisema wateja wa kampuni hiyo wanaweza wakashinda zawadi mbalimbali zikiwamo vifaa vya umeme kama majokofu, runinga, safari za mapumziko kwenda Dubai na Zanzibar, pesa zinazofikia mpaka Sh. milioni 30 kwa mteja mmoja na zawadi kubwa ya gari mpya.

"Kila mteja atakayeshinda zawadi yoyote, atakuwa na nafasi ya kumchagua mpendwa wake mmoja na yeye kushinda aina hiyo ya zawadi, atakayeshinda gari atamchagua mpendwa wake mmoja na yeye ashinde gari jipya na ndio maana tumetenga magari mawili kwenye kampeni hii," alisema Pesha.

Alisema kampeni hiyo itadumu kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia jana ambapo droo ya mwisho itachezeshwa Januari mwakani kwa mshindi wa gari.

## Yanga kurudia ya USM Alger kuimaliza CR Belouizdad kwao

INATOKA UK. 24

Shirikisho kwenye mechi hiyo ya fainali kutokana na matokeo mabaya ya nyumbani.

Alisema mbali na kufikia kwenye hoteli hiyo ambayo wanaona wana bahati nayo, wametumia mbinu zilezile kukwepa fitina za wenyeji wao kuelekea kwenye mchezo huo.

"Tumefikia kwenye hoteli ambayo mara ya mwisho tulikuja kucheza mechi yetu ya fainali dhidi ya USM Alger, inaonekana tuna bahati nayo, hii inatupa matumaini na nguvu kuwa tunaweza kupata matokeo mazuri. Tumerudi tena hapa, tutakuwa hapa hadi siku ya mechi yetu Ijumaa," alisema Kamwe na kuongeza,

"Yanga ni ile ile, hoteli ni ile ile na uwanja ni ule ule, lakini kikubwa tumetumia mbinu ile ile tuliyotumia dhidi ya USM Alger, kwa uwezo wa Mungu matokeo yatabaki vile vile," alisema Kamwe.

Yanga itakipiga katika Uwanja wa Juillet wa Tano jijini Algiers, ambao mara ya mwisho iliifunga USM Alger bao 1-0 lililofungwa kwa mkwaju wa penalti na Djuma Shaaban dakika ya saba ya mchezo, katika fainali hiyo iliyochezwa Juni 3 mwaka huu.

Akizungumzia kundi la pili la wachezaji, Kamwe alisema lilitarajiwa kuwasili leo baada ya majukumu ya timu ya taifa.

"Kundi la pili lilitarajiwa kuondoka leo (jana) baada ya majukumu ya timu ya taifa, unajua sisi wachezaji wetu wengi wanaocheza timu za taifa wapo Taifa Stars, kwa hiyo tunatarajia kesho (leo), watakuwa wamewasili," alisema Kamwe.

## Cadena: Tupo tayari kuwakabili Asec Mimosas

INATOKA UK. 24

hatuwezi kufanya hivyo bila shabiki bora kuwepo uwanjani, tuna uchungu na timu yetu na ili kuonyesha kweli tuna uchungu lazima tuisaidie timu kushinda Jumamosi.

Wabaya wetu wanawekeza nguvu kubwa kutukejeli ili tupoteze mwelekeo na mchezo wa Jumamosi tufanye vibaya, lakini Simba tumeshakuwa wakomavu, tutahakikisha tunapata ushindi mbele ya Asec Mimosas," alisema Ahmed.

Alisema wachezaji wamewaahidi kwenda kuipambania timu na kilichobaki mashabiki kwenda uwanjani kwa wingi siku hiyo kwa ajili ya kuwapa furaha.

Michezo
Alhamisi Novemba 23, 2023
Nipashe



## Miami yagoma Messi kukutana na Ronaldo

UKURASA 21

UZINDUZI...



Wachezaji wa Simba, Hussein Kazi, Moses Phiri na Che Malone wakiwa wamevaa jezi mpya za timu hiyo zilizozinduliwa jana kwa ajili ya michezo yao ya hatua ya Makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SIMBA**

# YANGA KURUDIA YA USM ALGER KUIMALIZA CR BELOUIZDAD KWAO

●●●Yatamba kuwafunga wenyeji wao nyumbani kama ilivyokuwa kwenye...

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga kimewasili salama nchini Algeria tayari kwa mchezo wake wa kwanza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CR Belouizdad huku wakitamba kupita njia zile zile ambazo ilizopita ilipocheza mechi ya fainali ya Kombe la Shirikisho msimu uliopita dhidi ya USM Alger na kuibuka na ushindi wa bao 1-0.

Yanga iliwasili juzi jijini Algiers ikiwa na baadhi ya wachezaji na huku wachezaji wengine walioikuwa kwenye majukumu ya timu zao za taifa wanategemea kuwasili leo tayari kwa mchezo huo utakaochezwa kesho.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Algiers, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema maandalizi ya mechi hiyo ya Kundi D yanakwenda vizuri ambapo mbali na wachezaji kuwa tayari kwa ajili mchezo huo kwa mbinu na kisaikolojia, lakini kitu kingine kinachowafanya wawe na uhakika wa ushindi ni kukaa kwenye hoteli ambayo walifikia wakati wanajiandaa kucheza dhidi ya USM Alger na kushinda mechi hiyo kwa bao 1-0, ingawa walishindwa kutwaa Kombe la

INAENDELEA UK. 23

## Cadena: Tupo tayari kuwakabili Asec Mimosas

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuifuatilia Asec Mimosas katika michezo yao miwili ya Ligi Kuu, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Daniel Cadena, amesema amegundua ubora na udhaifu wa wapinzani wao na sasa wapo tayari kukabiliana nao.

Simba inatarajia kuwa mwenyeji wa Asec Mimosas katika mchezo wa kwanza hatua ya makundi Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Cadena aliiambia Nipashe jana kuwa wapinzani wao hao wamecheza michezo mitano ya Ligi Kuu nchini kwao na kati ya hiyo wameshinda mechi mbili, wametoka sare mechi moja na kupoteza mechi mbili ambapo ameona sehemu yenye udhaifu.

"Tupo tayari sasa kukabiliana nao, utakuwa mchezo mzuri lakini naamini Simba itafanya vizuri, tumewafuatilia vya kutosha wapinzani wetu, tumeona wapi wapo imara na wapi tunaweza kutumia udhaifu wao kupata matokeo mazuri, tunataka kuanza vizuri kwenye hatua hii," alisema Cadena.

Alisema moja ya sehemu ambayo wapinzani wao hawapo vizuri ni sehemu ya ulinzi ambapo anaamini kwa safu ya Simba ya ushambuliaji wanaweza wakapata matokeo mazuri.

"Hili tatizo kwenye ulinzi na sisi tulikuwa nalo, lakini nashukuru tumelifanyia kazi na kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kuweka mambo sawa, hii inanipa matumaini ya kufanya vizuri Jumamosi," alisema Cadena.

Alisema kuna mabadiliko makubwa ndani ya kikosi chake na mashabiki watashangaa kwa namna walivyobadilika haraka.

Katika hatua nyingi Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, aliwataka mashabiki wa klabu hiyo kujitokeza kwa wingi Jumamosi kushangilia timu yao.

Alisema timu iko vizuri na wamedhamiria kushinda mchezo huo na hakuna timu yoyote ambayo inaweza kuwasumbua kwenye Uwanja wa Mkapa.

"Tumedhamiria kushinda na

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042